SportPesa
TZS. 667,771,400
NI YA KWAKO WIKI HII,
BETI LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#



**Kielelezo** cha Jamhuri chapingwa kupokewa katika kesi ya Mbowe

UKURASA 3



**Pjanic arejesha matumaini Barca**

UKURASA 23

Nipashe
Jumamosi Novemba 13, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580764
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US



# TWENDE HIVI

• **Serikali** yatoa msimamo mafao wastaafu, tahadhari ukame, bima ya afya kwa wote na bei ya mbolea... *Endelea ukurasa 2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 4
**KIGOGO TAKUKURU ASHINDA KESI UTAKATISHAJI FEDHA**
VILIO vya furaha vilitawala jana katika viunga vya Mahakama ya...

UKURASA WA 4
**VICHWA TRENI UMEME KUWASILI MWEZI HUU**
WAZIRI wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, amesema...

UKURASA WA 5
**DAR YAPOKEA MSAADA MAPAMBANO CORONA**
MKOA wa Dar es Salaam umepokea shehena ya makasha 500 ya vifaa...



Rais Samia Suluhu Hassan, akipata maelezo kuhusu uhifadhi wa nyaraka mbalimbali alipotembelea jengo jipya la Makumbusho, katika mji mpya wa serikali, Cairo, Misri juzi. **PICHA: IKULU**

## Ufafanuzi kuhusu hali ya mafuta

UKURASA 2



## Msako silaha kurindima nyumba kwa nyumba

UKURASA 3

Scan Hapa
Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu
Google Play App Store



MICHEZO **DAKIKA 90 CHUNGU ZILIZOIMALIZA STARS** UK.24
**MAONI, KATUNI** UK.6



Basi la abiria maarufu kama daladala linalofanya safari kati ya Tegeta Nyuki na Mbezi kupitia Madale, likiwa limepata ajali baada ya kumshinda dereva wake, katika eneo la Madale Nguzo, Manispaa ya Kinondoni, mkoani Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

# Serikali yasema twende hivi

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

SERIKALI imeagiza kutatuliwa haraka tatizo la ucheleweshaji wa mafao ya wastaafu katika mifuko ya hifadhi ya jamii, huku ikiitaka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kuhakikisha kuanzia mwaka ujao wa fedha, sheria ya bima ya afya kwa wote iwe imeanza kutekelezwa.

Katika hotuba yake ya kuahirisha Bunge jana, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, alimtaka Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Ajira, Uratibu na Watu Wenye Ulemavu), Jenista Muhagama, kushirikiana na Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, kuhakikisha vikwazo katika upatikanaji wa mafao ya wastaafu kwa wakati vinaondoka.

Majaliwa alisema: "Kuhusu mafao ya wastaafu namwelekeza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Ajira, Uratibu na Watu Wenye Ulemavu) kushirikiana na Waziri wa Fedha na Mipango kuhakikisha changamoto ya upatikanaji wa mafao ya wastaafu kwa wakati inaondoka."

**BIMA YA AFYA**

Kuhusu bima ya afya kwa wote, Waziri Mkuu alisema katika mkutano wa nne wa Bunge la 12, serikali iliahidi kuwasilisha Muswada wa Sheria kuhusu Bima ya Afya kwa Wote.

Alisema serikali inatoa umuhimu mkubwa kwenye suala hili sambamba na kuhakikisha masuala yote ya kisera, kisheria na kibajeti yanatazamwa kwa kina.

Majaliwa alisema hatua muhimu za awali zimekamika na sasa serikali inawashirikisha wadau wengi zaidi ili kutengeneza mfumo ambao hautokuwa na dosari nyingi.

Alisema lengo la serikali ni kuona utekelezaji wa suala hilo unaanza mwaka ujao wa fedha 2022/23, ili kila mwananchi awe na uhakika wa kupata matibabu kila inapolazimu.

Majaliwa alisema: "Hivyo basi, nitoe maelekezo kwa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kushirikiana na wadau wote muhimu katika kuhakikisha Muswada wa Sheria kuhusu Bima ya Afya kwa Wote unakamilika kwa wakati ili kukidhi malengo ya serikali na matarajio ya wananchi."

**UKUSANYAJI MAPATO**

Majaliwa pia alizungumzia ukusanyaji mapato ya ndani, akisema ni miongoni mwa maeneo yaliyoibua hoja wakati wa mkutano huo wa Bunge.

Aliiagiza Wizara ya Fedha na Mipango kushirikiana na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kuimarisha matumizi ya vifaa vya kielektroniki katika ukusanyaji wa mapato ya ndani ya serikali.

**RIBA BENKI**

Majaliwa pia alisema serikali imekuwa ikichukua hatua madhubuti kupitia Benki Kuu ya Tanzania (BoT) ikiwamo kupunguza kiwango cha akiba kinachowekwa na benki katika Benki Kuu.

Alisema serikali pia imekuwa ikichukua hatua ya kulegeza masharti ya uanzishwaji wa ofisi za wakala wa benki, kushusha riba inayolipwa kwa akaunti za fedha za mitandao pamoja na kutenga Sh. trilioni moja kwa ajili ya mikopo kwa benki na taasisi za fedha kwa riba ya asilimia tatu, ili benki na taasisi hizo zitoe mikopo kwa riba isiyozidi asilimia 10.

Alisema hatua hizo zinalenga kupunguza kiwango cha riba kwenye mikopo ya benki ya kibiashara na taasisi za fedha, kupunguza riba katika shughuli za kilimo kwa kiwango kisichozidi asilimia 10 na kuongeza kasi ya utoaji wa mikopo kwa sekta binafsi, ili kuchechemua shughuli za kiuchumi.

Hata hivyo, Majaliwa alisema kuwa licha ya hatua hizo, bado kumekuwa na dosari ya kutoshuka kwa kiwango cha riba kinachotozwa na benki na taasisi za fedha, Waziri Mwigulu akitolea ufafanuzi suala hilo juzi kuwa linatokana na kuwapo idadi ndogo ya wakopaji nchini.

"Kwa mantiki hiyo, ninaiagiza Wizara ya Fedha na Mipango ikutane na taasisi za fedha nchini kuona namna wanavyoweza kupunguza riba kubwa kwenye mikopo wanayotoa hususani kwa makundi ya wafanyabiashara na wajasiriamali wadogo," alisema Majaliwa.

## Ufafanuzi hali ya mafuta nchini

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKA la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) limetoa ufafanuzi kuhusu hali ya upatikanaji wa mafuta, likibainisha kuwa hakuna uhaba wa nishati hiyo nchini.

Taarifa iliyotolewa jana na Kitendo cha Uhusiano na Mawasiliano cha TPDC, pia ufafanuzi wa Mkurugenzi Mtendaji wa TPDC, Dk. James Mataragio, kwa Nipashe jana kuhusu kauli yake ya juzi, ilibainisha kuwa serikali imeweka utaratibu madhubuti wa uingizaji wa mafuta kuhakikisha nchi inakuwa na mafuta ya kutosha siku zote.

Kwa mujibu wa shirika hilo, kilichozungumzwa na mkurugenzi huyo katika warsha ya waandishi wa habari mkoani Dar es Salaam juzi, ni mikakati ya serikali kupitia TPDC kuongeza uwezo wa nchi kuhifadhi mafuta ya akiba kwa kipindi cha miezi mitatu hadi sita.

Shirika hilo lilibainisha kuwa mikakati hiyo itaifanya nchi kuwa na hifadhi ya mafuta kwa kipindi kirefu ili kuliweka taifa katika njia sahihi ya kuepuka dharura zinazoweza kujitokeza katika biashara ya mafuta duniani.

"Hivyo, ieleweke kwamba hakuna uhaba wa upatikanaji wa mafuta nchini, mafuta yapo na yataendelea kupatikana kwa wakati kwa kuwa meli za mafuta zimeendelea kuleta bidhaa hiyo nchini chini ya utaratibu unaoratibiwa na wakala wa serikali wa ununuzi wa mafuta kwa pamoja nchini (PBPA)," shirika hilo lilifafanua.

Jana Nipashe ilimnukuu Mkurugenzi Mtendaji wa TPDC akibainisha mafuta yaliyopo nchini kwa sasa yanatosha kwa matumizi ya siku 15, yaani wiki mbili pekee.

Hata hivyo, katika ufafanuzi wake wa jana, kiongozi huyo alibainisha kuwa alichokilenga ni kiwango cha akiba ya mafuta kilichopo nchini - kwamba kwa sasa wanayo akiba inayotosha siku 15 na mkakati uliopo unalenga kuifanya nchi kuwa na akiba ya kutosheleza miezi mitatu hadi sita.

# ...yataja hatua muhimu kuukabili ukame

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, amesema serikali imeanza kuchukua hatua mahsusi ili kukabiliana na athari zinazoweza kujitokeza kutokana na upungufu wa mvua.

Alitoa kauli hiyo jana bungeni wakati akiahirisha mkutano wa tano wa Bunge la 12 na kueleza kuwa hatua hiyo imetokana na taarifa ya Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA).

Katika taarifa ya TMA iliyotolewa Septemba mwaka huu, kulitabiriwa kuwa viwango vya mvua katika msimu huu wa kilimo vitakuwa vya wastani katika baadhi ya maeneo, hali imbayo itaathiri uzalishaji wa baadhi ya mazao.

Majaliwa alitaja hatua hizo ni pamoja na Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) kuendelea kununua chakula na kuhifadhi.

Pia alisema serikali itafuatilia kwa karibu mwenendo wa ukuaji wa mazao shambani sambamba na kufanya tathmini ya hali ya uzalishaji wa mazao ya chakula kwa msimu wa mwaka 2021/22.

UPATIKANAJI WA MBOLEA

Waziri Mkuu pia alisema kutokana na kusuasua kwa uagizaji wa mbolea nchini na ongezeko la bei kwa takribani asilimia 96 kulinganishwa na bei ya mwaka jana, serikali imechukua hatua za haraka kukabiliana na hali hiyo.

Majaliwa alitaja hatua hizo kuwa ni serikali kuwasiliana moja kwa moja na wazalishaji wa mbolea katika nchi rafiki ili kupata mbolea kwa gharama nafuu.

Pili, kuruhusu wafanyabiashara kuingiza mbolea nchini bila kutumia zabuni za mfumo wa ununuzi wa pamoja na kuuza kwa bei ya ushindani.

"Hatua hii imesaidia kuongeza kiwango cha mbolea kinachoingizwa nchini kati ya Julai na Oktoba 2021. Katika kipindi hicho, tani 48,400 za mbolea ya urea ziliingizwa nchini kulinganishwa na tani 33,948 zilinunuliwa kwa zabuni ya mfumo wa pamoja msimu wa 2020/21," alisema Majaliwa.

Hatua ya tatu aliitaja kuwa ni kuhamasisha matumizi ya mbolea mbadala wa DAP na urea kama vile NPK, NPS, NPSZinc, Nafaka+ ya Minjingu, mbolea za asili, chokaa na mbolea ya Fomi Imbura inayozalishwa na Kiwanda cha Fomi cha Burundi.

Alisema hatua nyingine ni kuhamasisha uwekezaji wa viwanda vya ndani vya kuzalisha mbolea ikiwa ni sehemu ya suluhisho la muda mrefu.

Alisema hatua ya tano ni kukamilisha mazungumzo na Serikali ya Burundi kuhusu kununua mbolea ya Fomi Imbura.

Majaliwa alisema hatua ya sita ni serikali kupitia Kampuni ya Mbolea Tanzania (TFC) imeshaagiza tani 20,000 za mbolea ya kupandia (DAP) na tani 60,000 za mbolea ya kukuzia (urea), itakayouzwa kwa gharama nafuu ambayo inalingana na uwezo wa wakulima.

Alisema hatua ya saba ni kukamilisha utafiti wa afya ya udongo katika mikoa ya Pwani, Dar es Salaam, Mtwara, Lindi, Tanga, Ruvuma, Tabora na Kigoma kwa lengo la kuwezesha viwanda vya mbolea hususani vilivyoko nchini kuzalisha mbolea kulingana na afya ya udongo sambamba na matumizi sahihi ya mbolea.

## HABARI KITAIFA

# Kielelezo kingine Jamhuri chapingwa kesi ya Mbowe

**Na Kulwa Mzee**

UPANDE wa utetezi katika kesi inayomkabili Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Freeman Mbowe na wenzake watatu, umepinga tena mahamakani kupokea kielelezo katika kesi ndogo ndani ya kesi ya msingi.

Kielelezo hicho ni barua kutoka kwa Msajili wa Mahakama na Wakili Peter Kibatala amedai kwamba asingependa Naibu Msajili, N. N. Ntundu, kutoa ushahidi kwenye kesi hiyo.

Amedai Msajili atahusishwa kuziba matundu, aulizwe alimkabidhi barua shahidi kwa madhumuni gani wakati shahidi si mhusika.

Wakili Kibatala alidai hayo jana katika Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi mbele ya Jaji Joackim Tiganga, wakati shahidi wa pili kwenye kesi ndogo, Koplo Msemwa akitoa ushahidi.

Kabla ya Kibatala, Wakili wa utetezi, Jeremiah Mtobesya, alipinga kupokewa barua hiyo kama kielelezo kwa madai kwamba inaonyesha mlengwa ni Ofisi ya Mashtaka ya Taifa na shahidi si mtumishi wa ofisi hiyo na hakujitambulisha hivyo.

Mtobesya aliungwa mkono na wakili mwenzake wa utetezi, John Mallya, ambaye alidai katika barua hiyo, wanaohusika ni Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) ambao ndio wanafanya huduma hizo za mashtaka na kwamba shahidi si mmojawapo.

Hatimaye Kibatala aliunga mkono pingamizi akidai kuwa shahidi hajaongozwa kwa namna yoyote kuhusu Ofisi ya Mashtaka ya Taifa, Sanduku la Posta 1733, Dodoma, ambaye anatambulika na mahakama afikishe kwa shahidi.

"Hatari ambayo tusingependa itokee ni Naibu Msajili N. N. Ntandu kuja kutoa ushahidi kwenye kesi hii.

"Mahakama itahusishwa kuja kuziba matundu, Msajili aje kuulizwa alimkabidhi shahidi DR kwa madhumuni gani wakati shahidi si mhusika," alidai Kibatala.

Akijibu hoja za pingamizi Wakili wa Serikali Mwandamizi, Abdallah Chavula, alidai hawakubaliani nazo kwa madai kwamba majina ya shahidi yamo katika barua hiyo pamoja na namba zake, hivyo nyaraka inamuhusu shahidi na kwamba barua haikutakiwa kwenda Ofisi ya Taifa ya Mashtaka.

"Shahidi anasema aliyempa barua ni Msajili. Katika ukurasa wa nyuma unaonyesha kina nani wanapaswa kupata barua hiyo na miongoni mwao shahidi ni mmojawapo.

"Kama tunaamini nyaraka inasema yenyewe tuache nyaraka hiyo ijisemee, je, iliandikwa kwa ofisi ya mashtaka Dodoma au kuna wengine?"alihoji Chavula.

Wakili wa Serikali, Pius Hillar, alipinga hoja za mawakili wa utetezi na kuiomba mahakama itupilie mbali pingamizi lao na ipokee kielelezo.

Awali, akiongozwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Robert Kidando, Msemwa alidai aliwahi kufanya kazi Kituo Kikuu cha Polisi Dar es Salaam kuanzia mwaka 2014 hadi 2021 alipohamishwa. Msemwa alidai kuwa miongoni mwa majukumu yake yalikuwa kufanya doria, misako na kufanya kazi katika chumba cha mashtaka.

Alidai kuwa Agosti 7, 2020 alikuwa zamu chumba cha mashtaka na aliwapokea watuhumiwa Adamu Kasekwa na Mohammed Ling'wenya ambao walifikishwa kituoni na ACP Ramadhan Kingai, SP Jumanne Malangahe na askari wengine wakiwa wameshika bunduki. Alidai kuwa watuhumiwa walikuwa wakituhumiwa kula njama kufanya vitendo vya kigaidi na alijaza majina yao, umri na afya zao kwenye kitabu cha kumbukumbu za watuhumiwa (DR). Alidai watuhumiwa walimweleza kuwa afya zao ni nzuri na akaandika 'good' kisha akawapeleka mahabusu na walipotolewa pia aliandika.

Shahidi alidai kuwa baadae Kasekwa alifuatwa na ACP Kingai na Ling'wenya alichukuliwa na SP Jumanne na kwamba kitabu cha kumbukumbu kilibaki kwa Mkuu wa Upelelezi Mkoa kwa ajili ya kuingiza taarifa za watuhumiwa wengine.

Kitabu hicho, alidai kuwa alikiona wakati mwingine Januari, mwaka huu, alipoitwa kwa ajili ya kutoa ushahidi.

Alidai kuwa watuhumiwa wakiwa mahabusu, alikuwa anawatembelea asubuhi, mchana na jioni na aliwapelekea chakula ikiwamo uji wa asubuhi.

"Watuhumiwa walipofikishwa Kituo Kikuu cha Polisi hakukuwa na mgonjwa. Kitabu cha kumbukumbu za watuhumiwa (DR) niliitoa mahakamani kama kielelezo Septemba 20, mwaka huu, wakati natoa ushahidi kwenye kesi ndogo mbele ya Jaji Siyani.

"Mheshimiwa Jaji, naomba kutoa barua inayothibitisha kwamba nilipokea DR kutoka kwa Msajili wa Mahakama. Barua hii ndio iliyonipa kielelezo hiki," alidai.

Mbali na Mbowe, washtakiwa wengine katika kesi hiyo ni Adamu Kasekwa, Mohammed Ling'wenya na Halfani Bwire. Wote wanakabiliwa na mashtaka sita likiwamo la kula njama kufanya vitendo vya kigaidi kati ya Mei Mosi na Agosti 5, 2020.




Mwenyekiti wa Taasisi ya Eden Twins, Diana Joy Mbena, akizungumza kwenye maadhimisho ya siku ya watoto mapacha, iliyoandaliwa na shirika hilo, Kijitonyama, Manispaa ya Kinondoni, mkoani Dar es Salaam juzi. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Msako silaha kurindima nyumba kwa nyumba

**Na Romana Mallya**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam limewataka wananchi wanaomiliki silaha kinyume cha sheria, kutumia fursa ya mwezi mmoja uliotolewa na serikali kuzisalimisha kwa kuwa baada ya hapo msako mkali wa nyumba kwa nyumba utafanyika.

Hivi karibuni Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene, alitoa tamko la msamaha unaoishia Novemba 30, mwaka huu kwa watu wanaomiliki silaha kinyume cha sheria kwa sababu mbalimbali ikiwamo kuisha muda wa kibali cha umiliki wake au kurithi, kuzisalimisha.

Jana Kamanda wa Kanda hiyoa, Jumanne Muliro, alisema kuwa baada ya muda huo uliotolewa na serikali, msako wa eneo kwa eneo, nyumba kwa nyumba utafanyika ukiongozwa na taarifa za kiintelijensia, lengo likiwa ni kuhakikisha wanaomiliki kinyume cha sheria, wanakamatwa na hatua kuchukuliwa.

Aliwakumbusha wanaosalimisha silaha hizo ndani ya muda uliowekwa, wazipeleke katika vituo vyote vya polisi, ofisi za serikali za mitaa na kwa watendaji wa kata kuanzia saa mbili asubuhi hadi saa 10 jioni.

Kamanda Muliro pia alisema katika mapambano ya matukio ya ukatili wa jinsia dhidi ya wanawake na watoto, Jeshi la Polisi katika kipindi cha kuanzia Januari hadi Oktoba mwaka huu, limefikisha mahakamani jumla ya kesi 43.

Alibainisha kuwa katika kesi hizo, zipo zilizotolewa hukumu, baadhi wamefungwa kifungo cha mpaka miaka 30 na faini ya fedha taslimu au vyote kwa pamoja.


MWENDOKASI AUCTION MART & COMPANY LIMITED
Head Office: P.O Box 1983 Dar es Salaam, Gongo la Mboto Majoe Street
Mobile: +255719 958094, +255653 123466
Branches: Nera Street Mwanza, Postal Road Dodoma,
Email: mwendokasiauctionmart@gmail.com/ mwendokasiauctionmart@yahoo.com

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA KWA WADAIWA SUGU WA SHIRIKA LA KUHUDUMIA VIWANDA VIDOGO (SIDO) MKOA WA KAGERA**

Kwa idhini tuliyopewa na mteja wetu Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) Mkoa wa Kagera, tutauza kwa njia ya mnada wa hadhara mali zilizoorodhesha hapa chini ambazo ziliwekwa kama dhamana ya mkopo. Minada itafanyika mahali zilipo mali hizo siku na saa kama zinavyoonyesha katika jedwali lifuatalo.

| S/No. | JINA LA MDAIWA | DHAMANA/MAHALI ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|
| 1. | MAXIMILIAN KATO | NYUMBA – KIBETA, BUKOBA MANISPAA | 04/12/2021 Siku ya Jumamosi Saa10:00 Asubuhi |
| 2. | MARIAM A. SAID | NYUMBA – KAYANGA, KARAGWE | 27/11/2021 Siku ya Jumamosi Saa10:00 Asubuhi |
| 3. | REGNARD M.SELESTINE | NYUMBA – KEMONDO, BUKOBA VIJIJINI | 28/11/2021 Siku ya Jumapili Saa10:00 Asubuhi |
| 4. | SPONSIOZA I.SIMON | NYUMBA – NSHAMBYA, BUKOBA MANISPAA | 05/12/2021 Siku ya Jumapili Saa10:00 Asubuhi |
| 5. | DANIEL T. BIIZA | NYUMBA – KASHAI, BUKOBA MANISPAA | 04/12/2021 Siku ya Jumamosi Saa13:00 Mchana |
| 6. | IVAN KAROL | NYUMBA – KASHAI, BUKOBA MANISPAA | 27/11/2021 Siku ya Jumamosi Saa13:30 Mchana |
| 7. | EDWINE MUSHOBOZI | NYUMBA–RWAMISHENYE, BUKOBA MANISPAA | 28/11/2021 Siku ya Jumapili Saa13:00 Mchana |
| 8. | BEATRICE KULINDA | NYUMBA – HAMUGEMBE, BUKOBA MANISPAA | 27/11/2021 Siku ya Jumamosi Saa11:30 Asubuhi |
| 9. | CLEOPATRA BISHANGA | NYUMBA – KASHAI, BUKOBA MANISPAA | 28/11/2021 Siku ya Jumapili Saa11:30 Asubuhi |
| 10. | SULEIMANI K.KATAI | NYUMBA – KAHORORO, BUKOBA MANISPAA | 28/11/2021 Siku ya Jumapili Saa10:00 Asubuhi |
| 11. | ANGELA T.NGAIZA | NYUMBA – HAMUGEMBE, BUKOBA MANISPAA | 27/11/2021 Siku ya Jumamosi Saa11:00 Asubuhi |
| 12. | GEOFREY JOHNSON JOHN | NYUMBA – KEMONDO , BUKOBA VIJIJINI | 05/12/2021 Siku ya Jumapili Saa10:00 Asubuhi |

**MASHARTI YA MNADA**

i. Mununuzi atalazimika kulipa 25% ya bei iliyofikiwa katika mnada,salio litalipwa ndani ya siku 14 toka tarehe ya mnada huo
ii. Endapo mnunuzi atashindwa kulipa salio kwa muda huo atakuwa amepoteza haki yake mnada utarudiwa 25% haitarejeshwa.
iii. Wateja wata ruhusiwa kukagua mali husika kabla ya mnada.
iv. Mali itauzwa kama ilivyo.
v. Gharama za usajili/ ubadilishwaji umiliki ni jukumu la mnunuzi.

**MWENDOKASI AUCTION MART & COMPANY LIMITED**
**KWA MAELEZO ZAIDI WASILIANA NA:-**
**MKURUGENZI MTENDAJI :**
**MOBILE :0686031825/0753121203**
**AU FIKA OFISI ZA SIDO MKOA WA KAGERA**

216568901

# Kigogo TAKUKURU ashinda kesi utakatishaji wa fedha

**Na Hellen Mwango**

VILIO vya furaha vilitawala jana katika viunga vya Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam, baada ya kumwachia huru Mhasibu Mkuu wa zamani wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Godfrey Gugai, na wenzake wawili. Kuachiwa kwa washtakiwa hao kulitokana na Jamhuri kushindwa kuthibitisha makosa 40 yakiwamo ya kutakatisha fedha na kumiliki mali za zaidi ya Sh. bilioni 3.6 tofauti na kipato chao.

Hukumu hiyo imesomwa jana katika Mahakama na Hakimu Mkazi Mkuu Thomas Simba, aliyekuwa akisikiliza kesi hiyo.

Mbali na Gugai, wengine ambao wameachiwa ni George Makaranga na Leonard Aloys.

Katika hukumu hiyo, Hakimu Simba alisema ushahidi uliotolewa na Jamhuri wa mashahidi 42, umeshindwa kuthibitisha makosa yote 40 yaliyokuwa yanawakabili washtakiwa hao. "Kuhusu shtaka la kukutwa na mali inayozidi kipato dhidi ya Gugai, mahakama yangu bila kuacha shaka imeona Jamhuri wameshindwa kuthibitisha tuhuma hizo. Jamhuri wameshindwa kueleza Gugai alikuwa anafanya shughuli gani kabla ya kuajiriwa na TAKUKURU, hivyo mwenye jukumu la kuthibitisha ni upande wa mashitaka.

"Mahakama hii inawaachia huru washtakiwa wote, hawana hatia," alisema Simba huku Gugai akionekana akipiga ishara ya msalaba akiwa kizimbani.

Akizungumza nje ya mahakama baada ya hukumu, Wakili wa utetezi, Alex Mgongolwa, alisema mahakama ni chombo cha haki, imesikiliza pande zote mbili na imezingatia sheria, hivyo wameridhika na uamuzi huo.

Katika kesi hiyo, awali upande wa Jamhuri uliongozwa Wakili wa Serikali Mkuu, Awamu Mbwagwa (kwa sasa ni Jaji wa Mahakama Kuu) akisaidiana na Mwendesha Mashtaka wa TAKUKURU, Maghela Ndimbo.

Mapema mahakamani hapo, washitakiwa walikuwa wanakabiliwa na makosa 40, kati ya hayo 19 ni ya kughushi, 23 ni utakatishaji fedha na moja ni kumiliki mali zilizozidi kipato halali, ambalo linamkabili Gugai.

Ilidaiwa kuwa mshitakiwa akiwa Dar es Salaam kama mwajiriwa wa TAKUKURU, alikuwa akimiliki mali za zaidi ya Sh. bilioni 3.6 ambazo hazilingani na kipato chake cha awali na cha sasa, huku akishindwa kuzitolea maelezo.



Ofisa Mkuu wa Huduma za Kifedha wa Tigo Pesa, Angelica Pesha, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, baada ya kutiliana saini makubaliano na Kampuni ya Norway inayoitwa Wakandi Group AS, ili kurahisisha huduma za kifedha kidigitali kupitia Tigo Pesa kwa SACCOS na taasisi ndogondogo za kifedha. Kushoto ni Mkurugenzi Mkuu wa Wakandi, Espen Kvallend. **Habari Uk. 8.** **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Vichwa treni umeme kuwasili mwezi huu

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, amesema serikali tayari imetia saini mkataba wa ununuzi wa vichwa viwili vya treni za umeme na mabehewa 30, vyote vinatarajiwa kuwasili nchini mwezi huu.

Kadhalika, amesema majaribio ya kwanza ya reli ya kisasa ya mwendokasi yamepangwa kufanyika Desemba mwaka huu.

Prof. Mbarawa alibainisha hayo jana jijini Dodoma wakati akitoa taarifa kwa waandishi wa habari kuhusu mafanikio ya sekta ya ujenzi na uchukuzi katika kipindi cha miaka 60 ya uhuru wa Tanganyika.

Alisema vichwa hivyo viwili vya treni ya umeme pamoja na mabehewa 30 vitawasili nchini mwezi huu kwa ajili ya kufanyika kwa majaribio ya kwanza ya reli ya kisasa ya SGR.

"Majaribio ya reli hii ya kisasa yamepangwa kufanyika Desemba, hivyo tusingeweza kufanya majaribio bila kuwapo kwa vifaa hivi. Kwa hiyo, ndani ya mwezi huu, tunavipokea vichwa hivyo pamoja na mabehewa hayo," alisema Prof. Mbarawa.

Alisema mkataba kwa ajili ya ununuzi wa vichwa vya treni za umeme 17 seti 10 za treni za umeme za abiria (EMU) pia ulitiwa saini na Julai 14, mwaka huu na vinatarajiwa kuwasili baada ya miezi 34.

"Na mkataba kwa ajili ya ununuzi wa mabehewa 59, ya abiria uliosainiwa tarehe 23, Septemba 2020, malipo ya awali yameshafanyika na hadi Juni, 2021 kazi ya matengenezo imefikia asilimia 45," alisema

Kadhalika, alisema mkataba huo ni wa miaka miwili ambao utakamilika Septemba 22, 2022 na taratibu za ununuzi wa mabehewa 1,430 ya mizigo zinaendelea.

Vilevile, alisema serikali kupitia Shirika la Reli Tanzania (TRC) ipo kwenye maandalizi ya kuanza ujenzi wa reli ya SGR, awamu ya pili kwa kipande cha Tabora-Kigoma kilomita 411, Kaliua-Mpanda-Karema Kilomita 321,Keza-Ruvuma kilomita 36, Isaka-Rusumo kilomita 371 na Uvinza-Musongati kilomita 240.

"Upembuzi yakinifu na usanifu wa awali wa vipande hivi umekamilika na hatua inayoendelea ni kuandaa makabrasha ya zabuni," alisema.

Waziri huyo alisema katika kukabilina na tabia ya makandarasi kujenda barabara chini ya viwango, serikali imenunua gari maalum ambalo litatumika kupima viwango vya ubora kila hatua.

"Tayari tumeshanunua gari ambalo inajulikana kama Road Scaner ambalo litakuwa linapima ubora wa viwango vya barabara kila hatua ili kuondokana na malalamiko," alisema Prof. Mbarawa.

Alisema serikali ipo katika mpango wa kubadilisha mizani yote ya upimaji magari na kufunga ya kisasa ambayo itaondoa malalamiko yaliyopo hivi sasa.

Alisema mizani inayotumika hivi sasa imekuwa ikilalamikiwa na watu wengi katika maeneo mbalimbali kutokana na mifumo yake ambayo imekuwa ichangia uwapo wa faini mbalimbali kwa madereva.

"Tunajipanga kufunga mizani ya kisasa katika maeneo yote ambayo itakuwa inapima gari likiwa linatembea na moja kwa moja Wakala wa Barabara (TANROADS) wanaona na sisi wizara tunaona wakati huo huo," alisema.

# Wenye mapacha wazipaza sauti

**Na Sabato Kasika**

WAZAZI na walezi wenye watoto mapacha, wameomba serikali kutambua vikwazo vinavyowakabili vikiwamo vya kushindwa kuwahudumia kutokana na hali duni ya kimaisha, ili waondokane navyo.

Waliotoa ombi hilo katika kilele cha maadhimisho ya Siku ya Kutambua Mapacha yaliyofanyika kwenye viwanja vya TCCL Kijitonyama, Dar es Salaam jana.

Maadhimisho hayo yaliandaliwa shirika lisilo la kiserikali la Eden Twins Foundation, na kushirikisha wadau mbalimbali kutoka mikoa ya Dar es Salaam na Pwani.

Saida Gaddafi, mkazi wa Dar es Salaam, ambaye analea mapacha wa binti yake, alisema familia zenye mapacha zinakabiliwa na vikwazo vingi hasa vya kiuchumi, hali ambayo inasababisha zishindwe kuwahudumia.

"Ombi kwa serikali ni kwamba, izione familia hizi kuwa ni zenye uhitaji muhimu na kuzisaidia kama inavyosaidia makundi mengine, kutokana na ukweli kwamba nyingi zina hali duni kimaisha," alisema.

Kwa muda mrefu, alisema kumekuwapo na mashirika mengi yasiyo ya kiserikali yanayohudumia makundi mbalimbali, na kwamba kwa upande wa familia za watoto mapacha ni Eden Twins Foundation pekee yake.

"Ninaomba serikali na wadau wengine kuunga mkono juhudi za Eden Twins Foundation kwani huku nako familia nyingi zinateseka kwa kushindwa kuwahudumia watoto wao," alisema.

Zainabu Mlazi, mkazi wa Mkuranga mkoani Pwani, mwenye mapacha tisa alisema anaishi kwa shida kutokana na kwamba anashindwa kuwatimizia watoto wake mahitaji yao ya kila siku.

"Mimi ni mjane, nimeachiwa watoto 10 wakiwamo mapacha tisa, ninaishi nao mwenyewe kwa kusaidiwa na wasamaria wema wakiwamo Eden Twins Foundation, ninaomba serikali itutambue na kutusaidia," alisema.

Kuhusu watoto hao, alisema uzazi wa kwanza hadi wa tatu, alikuwa anajifungua watoto wawili wawili na kujikuta ana watoto sita na kwamba uzazi wa nne akajifungua mmoja wakawa saba.

"Uzazi wa tano nimejifungua mapacha watatu wa kike, hivyo nina jumla ya watoto 10, ambao ninahangaika kuwalea katika maisha yangu haya ambayo kiuchumi si mazuri," alisema.

Mwenyekiti wa Eden Twins Foundation, Diana Joy Mbena, alisema alianzisha asasi hiyo ili kusaidia kuitambulisha vikwazo vinavyozikabili familia zenye watoto mapacha ili serikali na jamii ivijue na kusaidia kuvitatua.

"Eden Twins Foundation bado ni changa ndiyo mara ya kwanza kufanya maadhimisho kwa lengo la kutaka kuweka wazi maisha ya familia hizo kwamba ni magumu zinahitaji kusaidiwa," alisema Diana.

Alisema, maadhimisho hayo pia yalilenga kuhamasisha jamii kuzisaidia familia zenye watoto hao, kwa madai kwamba, nyingi inaishi maisha duni, haziwezi kulipia gharama za matibabu, chakula na hata mahitaji mengine muhimu.

# Dar yapokea msaada mapambano corona

**Na Moshi Lusonzo**

MKOA wa Dar es Salaam umepokea shehena ya makasha 500 ya vifaa tiba kwa ajili ya kupambana na ugonjwa wa corona katika hospitali mbalimbali.

Vifaa tiba hivyo vyenye thamani ya Sh. milioni 164, zikiwamo mashine za Oxjen na vifaa vya kujikinga wafanyakazi wa afya, vimetolewa na taasisi zisizo za kiserikali za An Nahl Trust, Nice Tanzania na NAMA Foundation ya Malasia.

Akizungumza wakati akipokea msaada huo, Katibu Tawala wa Mkoa wa Dar es Salaam, Hassan Rugwa, alisema vifaa hivyo vimetolewa katika muda mwafaka kutokana na hospitali nyingi kuwa na uhaba wa vifaa tiba.

Rugwa alisema kutokana na serikali kuendelea kupanua huduma za afya kwa kujenga hospitali mpya, mkoa unakabiliwa na uhaba wa vitendea kazi yakiwamo magari ya wagonjwa baada ya wagonjwa wengi kuhitaji huduma za haraka na zenye usahihi.

"Vifaa tiba hivi vitapunguza uhitaji katika hospitali zetu lakini tutaendelea kuhitaji kutokana na hospitali zetu mpya tulizojenga kutokuwa na uwezo wa kutosha hasa magari ya wagonjwa ambao wanahitaji huduma za haraka kunusuru maisha yao," alisema Rugwa.

Mratibu Mkuu wa Mradi huo, Hamza Jabir, alisema wametenga Sh. milioni 500 kwa ajili ya kununulia vifaa tiba katika hospitali za mkoa huo kwa ajili ya kupambana na corona.

"Vifaa vyote tumenunua kutoka Bohari Kuu ya Dawa (MSD). Wameanza kutoa sehemu ya shehena na kiasi kilichobaki kitatolewa mara tutakapokabidhiwa kwa ajili ya kusambaza katika hospitali zetu za Dar es Salaam," alisema.

Jabir alisema lengo la kutoa msaada huo ni kuunga mkono serikali katika mapambano yake dhidi ya ugonjwa huo na kunusuru maisha ya Watanzania.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Dk. Rashid Mfaume, alizishukuru taasisi hizo na kuahidi kutumika katika malengo yaliyokusudiwa na kuwafikia wale wote wenye uhitaji.

Kuhusu corona, Dk. Mfaume alisema bado hospitali zina wagonjwa wa maradhi hayo na kuwashauri watu kufuata kanuni za afya katika kujikinga na maambukizi mapya.




Mkuu wa Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE), Prof. Emmanuel Mjema akizungumza kwenye kongamano la wanataaluma wa chuo hicho, jijini Dar es Salaam jana, kabla ya mahafali yanayotarajiwa kufanyika chuoni hapo leo. Habari Uk. 8. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Serikali yaanika hali ukatili kijinsia nchini

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

SERIKALI imesema takwimu za vitendo vya ukatili kwa watoto vilivyoripotiwa katika vituo vya polisi zinaonyesha watoto 6,168 walifanyiwa vitendo hivyo kuanzia Januari hadi Septemba mwaka huu.

Imesema kati yao, wa kike ni 5,287 na wa kiume ni 881, huku waliobakwa ni 3,524, waliolawitiwa ni 637 wakiwamo wa kiume 567 na wanawake ni 70, waliochomwa moto ni 130 (wanaume 33 na wanawake 97), waliopata mimba ni 1,877.

Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Khamis Hamza Chilo, aliyasema hayo jana bungeni wakati akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum, Ester Matiko.

Akiuliza swali, Matiko alisema: "Ukatili kwa watoto umekithiri nchini kama vile ubakaji, ulawiti, kuchomwa moto na mimba za utotoni. Je, ni watoto wangapi wamefanyiwa ukatili huo kwa jinsia zao wa kike na wa kiume. Je, kuna takwimu halisi ya hatua zilizochukuliwa na serikali dhidi ya matukio hayo nchini?"

Akijibu swali hilo, Chilo alisema kuanzia Januari hadi Septemba mwaka huu, takwimu ya vitendo vya ukatili kwa watoto vilivyoripotiwa vituo vya polisi inaonyesha jumla ya watoto 6,168 wamefanyiwa ukatili. Alisema kati yao wanawake ni 5,287 na wanaume 881, waliobakwa ni 3,524, waliolawitiwa ni 637 kati yao wanaume 567 na wanawake 70, waliochomwa moto ni 130, kati yao wanaume 33 na wanawake 97 na waliopata mimba ni 1,877. Alisema kesi na watuhumiwa waliokamatwa na kufikishwa mahakamani ni 3,800, kesi zilizo chini ya upelelezi ni 2,368 na kesi zilizohukumiwa ni 88 na nyingine ziko kwenye hatua mbalimbali mahakamani.

Katika jitihada za kuzuia na kutokomeza vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto, Naibu Waziri huyo alisema serikali imeanzisha madawati ya jinsia na watoto katika vituo vya polisi ambapo hadi sasa zaidi ya madawati 420 yameanzishwa na yanafanya kazi kwa lengo la kuwawezesha waathirika kupata huduma stahiki katika vituo vya polisi na kutendwa haki.

# Ma- RC, ma-DC wadaiwa kikwazo utendaji kazi madalali mahakama

**Na Hellen Mwango**

VIONGOZI wa kisiasa, wakuu wa mikoa na wilaya wamedaiwa kuwa kikwazo katika utendaji kazi wa maofisa utekelezaji wa amri za mahakama (madalali wa mahakama) wanapotimiza majukumu yao.

Madai hayo yalitolewa jana Dar es Salaam na Mwenyekiti wa Mpito Chama cha Madalali Tanzania, Mwamvua Kigulu, wakati akitoa taarifa katika mkutano mkuu wa kwanza wa chama hicho.

"Leo (jana) tunafanya Mkutano Mkuu wa kwanza kwa madalali 55 kati ya 81 waliosajiliwa, lakini katika utekelezaji wetu majukumu tunakabiliwa na matatizo kutoka kwa baadhi ya viongozi wa siasa, wakuu wa mikoa na wilaya kutuzuia kufanya kazi," alisema.

"Dalali anaweza kufika eneo la kazi mara akazuiwa na amri ya mkuu wa mkoa au wilaya kwamba mpaka waanze kuita tena pande zote mbili kuwasikiliza kitu ambacho ni kinyume cha amri husika, hivyo kumsababishia mnufaika kukosa haki yake kwa wakati kama mahakama ilivyoamuru," aliongeza.

Kigulu alisema madalali sasa wako kisheria na kwamba wanapopewa kufuatilia utekelezaji wa amri ya mahakama, wanatakiwa kutoa taarifa kinapotokea kizuizi kutoka kwa viongozi hao kwa kuwa wanakuwa wameingilia amri husika.

Akifungua mkutano huo, Mtendaji wa Mahakama za Mwanzo, Humphrey Paya, alisema mahakama ilianzisha sheria na kuwasajili madalali nchini wale wenye sifa ikiwamo kuhudhuria masomo katika Chuo cha Uongozi wa Mahakama (IJA) kilichoko Lushoto, mkoani Tanga.

Mbali na kuhudhuria masomo katika chuo hicho, alisema mahakama sasa ina lengo la kuwasajili katika mfumo wa dijitali kama ilivyo kwa mawakili wa kujitegemea.

"Mahakama imefanya maboresho kuondoa kanjanja (wavamizi) wa udalali nchini. Ili usajiliwe ni lazima upate mafunzo katika chuo chetu cha IJA na kwamba tuko kwenye mchakato wa kuwaingiza kwenye mfumo wa digitali ili wananchi wapate huduma popote walipo na kwa uhakika," alisema Mtendaji Paya.

Alisema lengo hasa la kusajili madalali ni kusaidia makundi maalum wakiwamo wanawake, watoto na wenye ulemavu katika kupata haki zao.

Naye Mkuu wa Kitengo cha Madalali wa Mahakama nchini, Hakimu Mkazi Mkuu Richard Kabate, alisema mahakama iko karibu na madalali kwa sababu ni watendaji wakuu mara tu amri inapotolewa na inatakiwa kutekelezwa. Alisema mbali na mahakama pia madalali wanaruhusiwa kufanya kazi nyingine ikiwamo za benki.

"Hawawezi kusubiri kazi za mahakama kwa sababu wana vibali vya kufanya kazi kama madalali na si kanjanja wanaruhusiwa" alisema Hakimu Kabate.

Mkutano huo Mkuu wa kwanza tangu kuanzisha usajili wa madalali wa mahakama na umejumuisha madalali wa mikoa yote nchini.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ziara ya Sanjay Dutt ilete mageuzi tasnia ya filamu

**KAZI** iendelee, hii kauli inatakiwa iendelee kuzunguka na kuonekana kwa vitendo kwenye vichwa vya Watanzania wote ili kuhakikisha ndoto zetu zinatimia.

Kama ambavyo kwa upande wa mchezo wa mpira wa miguu, ndoto kubwa ya kila taifa ni kuona wanataka tiketi ya kushiriki katika mashindano makubwa ambayo si mengine bali ni fainali za Kombe la Dunia.

Fainali hizo kuchezwa kila baada ya miaka minne, lakini hutanguliwa na fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON), ambazo pia hujumuisha timu zilizo imara kutoka kwenye bara letu.

Wachezaji huandaliwa na nchi huweka mikakati ili kufikia ndoto hizo, lakini kuna wakati suala la bahati huchukua nafasi yake licha ya kila nchi kufanya maandalizi yaliyo bora na vikosi vyake kuundwa na wachezaji nyota.

Tukirudi katika upande wa sanaa ya filamu nchini, mapema wiki hii taifa lilipokea msanii mkongwe wa filamu, Sanjay Dutt ambaye ni raia wa India.

Tunaamini ziara ya mwigizaji huyo mkongwe haukuja kwa bahati mbaya, ujio wake unatakiwa kutumika kama sehemu ya darasa la kuwafundisha wasanii wetu kutoka hapa walipo na kufika kwenye daraja lingine.

Umefika wakati wasanii wa filamu Tanzania wakaamka na kutengeneza kazi ambazo zitalenga soko la kimataifa na hilo linawezekana kama watakubali kuwekeza katika kiwango cha juu.

Bila ya uwekezaji imara na wa kiwango kikubwa lakini wenye malengo, wasanii wa filamu wa hapa nchini wataendelea kuwa wasindikizaji kwenye tasnia hiyo inayotengeneza idadi kubwa ya ajira kwa watu wa rika mbalimbali.

Wasanii wanatakiwa wafahamu kuandaa kazi zenye ubora ndio zitapelekea kupata matunda mazuri sokoni na kufanya kazi kwa kuripua, watajiweka katika nafasi za chini na baadhi yao huweza kuichukia sanaa hiyo kutokana na kushindwa kumudu gharama za kujiendesha.

Dutt ambaye alipata nafasi ya kuonana na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa ameahidi kushirikiana na wasanii wa Tanzania katika kuleta mapinduzi ya kazi wanazozifanya ili zitambulike kimataifa.


Kupitia kwa mafanikio ambayo ameyapata msanii huyo mkongwe, hata wasanii na wadau wa tasnia ya filamu wa hapa nchini wanaweza kufikia ndoto zao endapo watafanya kazi zao kwa weledi na kuacha kuiona tasnia hiyo ni sehemu ya kupatia umaarufu.

Inafahami wazi kazi ya sanaa 'inalipa' na kama hilo ni kweli, basi wasanii wetu ambao walipata nafasi ya kuzungumza na mkongwe huyo kufanya mabadliko kwenye kazi zao na hatimaye tutashuhudia filamu zilizotengenezwa na kuandaliwa na wasanii wetu zikishinda tuzo mbalimbali za kimataifa.

Tuzo hizo haziendi bure, zitaenda sambamba na soko la dunia na hatimaye pia jina la nchi litapata heshima kupitia kazi za wasanii hao kama ambavyo wanataaluma wengine wamekuwa wakipeperusha vyema bendera ya nchi kupitia vipaji walivyonavyo.

Hakuna kinachoshindikana, kikubwa ni wadau wa tasnia ya filamu kukubali kwenda na kasi ya ushindani iliyopo katika dunia hii ya kidijitali.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Mchimba Kisima huingia mwenyewe

Na Barnabas Maro

**MTU** anayemchimbia mwengine shimo kwa dhamira mbaya huishia kuingia yeye mwenyewe!

Methali hii huweza kutumiwa kumshauri mtu anayekusudia kumfanyia ubaya mwenzake huenda ubaya huo ukamrudia yeye.

Nchi ni eneo la ardhi lenye utawala wake dola, yaani utawala wa nchi. Bendera ni kitambaa mahusus chenye rangi na alama maalumu ikiwa ni kitambulisho cha mamlaka fulani kama vile nchi au chama.

Ndio maana kila nchi duniani ina bendera ya aina tofauti zenye maana tofauti na za nchi zingine.

Bendera ya Tanzania ina rangi nne tofauti : Rangi ya bluu ina maana ya bahari kumaanisha Tanzania inapakana na Bahari ya Hindi. Rangi nyembamba ya njano maana yake ni madini yaliyo nchini mwetu ilhali rangi nyeusi inawatambulisha wananchi wa Tanzania kisha rangi ya kijani yaonyesha hali ya nchi ilivyo.

Hii yanikumbusha walivyosema wahenga kuwa: "Kila mlango una wimbile." Kwa kawaida kila mlango wa bahari una wimbi lake. Ni methali ya kutumiwa kutukumbusha kila kitu kina sifa zake tofauti hamna kinachofanana na kingine. Hatuwezi kufananisha hali tofauti.

Hukereka (sumbuliwa na jambo; chukizwa) sana nionapo timu zetu za taifa zinapopambana na timu ngeni zinapokuja nchini, wanaohudhuria kuwashangilia wachezaji wetu huwa wachache sana.

Kinachoshangaza ni kwamba Yanga na Simba zinapopambana kwenye uwanja wowote humu nchini baadhi ya mashabiki na wanachama wao huenda mkoa wowote ili kuzishangilia. Wengine hutumia baiskeli kwa mwendo unaowachukua siku kadhaa!

Ina maana Yanga na Simba ni bora kuliko timu za Taifa ambazo nazo huwa na mchanganyiko wa wachezaji wa timu nilizotaja hapo juu? Kama Yanga , Simba na Taifa Stars ni timu za nchi moja iitwayo Tanzania kwa nini twazithamini Yanga na Simba za mkoa mmoja tu kati ya mikoa takribani (kwa kukisia) 31?

Neno "Ujahili" lina maana ya ukatili; unyama; uonevu; upumbavu na ujinga. Kumbe baadhi yetu ndivyo tulivyo!

> **Kinachoshangaza ni kwamba Yanga na Simba zinapopambana kwenye uwanja wowote humu nchini baadhi ya mashabiki na wanachama wao huenda mkoa wowote ili kuzishangilia. Wengine hutumia baiskeli kwa mwendo unaowachukua siku kadhaa!**

Timu ngeni zinapokuja kucheza kwetu na kuona jinsi tunavyozishangilia ilhali Simba na Yanga ni zetu hutucheka kimoyomoyo na kuwaongezea nguvu za kucheza dhidi ya timu zetu. Pukachaka! (neno lenye kuashiria kutema mate ambalo humaanisha kukidharau kitu kilichotajwa.)

Kwa nini Simba na Yanga zinawekeana chuki yaani hali ya kutokuwepo upendo, hali ya kuwa na roho mbaya hali ya kuwa na kinyongo ilhali zote ni timu za mkoa wa nchi moja?

Kufarikiana (kitendo cha watu kutengana kutokana na kutoelewana) isiwe sababu ya kuwekeana chuki na kushangilia mojawapo zinaposhindwa na timu ngeni kutoka nnje ya Tanzania!

Tunapaswa kutambua "wajinga ndio waliwao." Kwamba ndio wanaopumbazwa au kuliwa. Methali hii huweza kutumiwa kumpigia mfano mtu ambaye ameishia kudanganywa kwa njia inayoonekana kuwa rahisi sana.

Simba na Yanga zapaswa kusoma kwa makini methali hii: "Ulimwengu ni dhaifu siuoneni sheshe" (kivumishi chenye maana ya kizuri kama vile 'nguo sheshe' ni nguo nzuri.)

Maana yake dunia au ulimwengu ni kitu dhaifu tusivutwe na sura yake ya uzuri. Methali hii hutumiwa kumtaadharisha mtu anayejisifu na kujigamba kutokana na uwezo au nguvu alizonazo ajue kwamba ulimwengu unaweza kumwangamiza.

"Chako ni chako, cha mwenzako si chako." Maana yake kitu unachokiita chako ni kizuri na huweza kukufaa na una uhuru nancho kuliko cha mtu mwingine.

Tunafunzwa tuvitegemee vitu vyetu wala sio vya watu wengine. Pia tunakumbushwa kuvithamini vitu vyetu ingawa sio vizuri kama vya wengine.

**marobarnabas@yahoo.com**
**0784 334 096**

HABARI KITAIFA

# Waziri ahimiza wanufaika wa TASAF kupata chanjo corona

**Na Mwandishi Wetu,** KONGWA

NAIBU Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Deogratius Ndejembi, amewataka wanufaika wa Mpango wa

Kunusuru Kaya Maskini wa Kijiji cha Songambele wilayani Kongwa kujitokeza kwa wingi kupata chanjo ya ugonjwa wa corona kwa kuwa chanjo hizo ni salama na itawasaidia kulinda afya itakayowawezesha kutumia vyema ruzuku wanayoipata katika shughuli mbalimbali za kiuchumi ili kuboresha maisha yao.

Ndejembi alitoa wito huo jana kwa wanufaika wa huo unaoratibiwa na Mfumo wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) akiwa wilayani Kongwa kwenye ziara ya kikazi ya kukagua utekelezaji wa shughuli za mpango huo zilizo chini ya ofisi yake.

Alisema ni jambo lisilokubalika kwa mlengwa wa TASAF ambaye bado hajapata bima ya afya kukataa chanjo ya corona inayotolewa bure na serikali halafu baadaye apate maradhi hayo na kulazimika kutumia fedha anayoipata kwa ajili ya matibabu.

"Mnufaika wa TASAF asiye na bima ya afya, atakayekataa chanjo ya corona na kupata ugonjwa huo, ataanza kuumwa, hivyo fedha ya TASAF atakayoipata kwa ajili ya kuboresha maisha yake, atalazimika kuitumia kwa matibabu," alifafanua.

Akizungumzia upotoshwaji unaofanywa kuhusu athari za chanjo ya corona, Ndejembi alisema wananchi wasidanganyike na propaganda zinazofanywa na wenye nia ovu kwa kuwa chanjo inayotolewa na serikali kwa wananchi wake imethibitika kuwa ni salama kiafya.

"Mimi binafsi nimechanja na mnaniona nipo mbele yenu nikiwa mzima wa afya, sijafa au kunyonyoka nywele kama wapotoshaji wanavyosema," Ndejembi alisisitiza.

Akihimiza matumizi mazuri ya ruzuku inayotolewa na TASAF, Katibu wa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Kongwa, Emmanuel Msemwa, aliwataka walengwa wa TASAF kuhakikisha fedha wanazozipata zinawasaidia kuanzisha miradi ya kiuchumi itakayoboresha maisha yao.

"Fedha mnayoipata kupitia Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini msiitumie kunywea pombe au kununulia vitu visivyo na msingi wowote kwenye magulio, ambavyo haviwasaidii katika kujenga uchumi," alionya.

Ndejembi jana alihitimisha ziara yake kikazi ya siku nne ya kukagua utekelezaji wa Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini katika Wilaya ya Chamwino na Kongwa.




Mkurugenzi wa shughuli za Mabenki wa Benki Kuu ya Tanzania, Agaton Kipangule (kulia), akipata maelezo kutoka kwa Meneja Uendeshaji wa Kampuni ya Tanzania Assurance Ltd, Ankit Babla (katikati), kuhusu huduma kwa wateja zitolewazo na kampuni hiyo, katika maonyesho ya wiki ya huduma za fedha kitaifa kwenye Viwanja vya Mnazi Mmoja, jijini Dar es Salaaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# DART waahidi maboreshomakubwa ya mwendokasi

**Na Romana Mallya**

WAKALA wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART) umesema baada ya kubaini ubora wa huduma na tija ipo chini ya viwango katika huduma hiyo kupitia falsafa ya maboresho endelevu, watumiaji wa huduma hiyo wataona mabadiliko ikiwa ni pamoja na abiria kutokaa muda mrefu vituoni.

Mtendaji Mkuu wa DART, Dk. Edwin Mhede, aliyasema hayo jana katika mafunzo ya watumishi wa DART yaliyofanyika mkoani Dar es Salaam.

Dk. Mhede alisema katika kufanikisha hilo, wametafuta machampioni wa kuendeleza falsafa ya KAIZEN yenye maana ya 'Maboresho Endelevu' ili kujenga uchumi imara wa sekta hiyo.

"Wizara ya Viwanda na Biashara kwenye hili tunaomba tuwashukuru Katibu Mkuu aliridhia, ana timu yake ambayo inaendeleza falsafa ya maboresho endelevu," alisema.

Alibainisha kuwa mbinu hiyo ya KAIZEN imekwenda kwenye sekta za uzalishaji, za umma mojawapo ni afya, nishati na usimamizi wa kodi na kwa mara ya kwanza nchini wanaitumia katika sekta ya usafirishaji ili inufaike nayo.

Dk. Mhede alisema wanataka kuona wateja wao hawakai muda mrefu kituoni kusubiria basi.

"Ndiyo maana ya mafunzo haya ya leo, hatujifunzi peke yetu hapa, wapo wabia na washirika wetu, kampuni ya UDART tumewaambia na wapo tayari kutekeleza," alisema.

Pia alisema falsafa hiyo inakwenda kuondoa upotevu wa muda wa wafanyakazi wawapo kazini ili kuongeza kasi ya utendaji kazi na kuhudumia wateja wa ndani na nje.

Mkurugenzi wa Maendeleo ya Viwanda, Lugano Wilson, aliishukuru Serikali ya Japan kupitia Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Japan (JICA) kwa ufadhili wao kwenye shughuli za KAIZEN katika uongezaji endelevu wa tija na ubora ili kujenga uchumi imara.

"Hivi karibuni wizara ilipokea na kuridhia maombi ya DART ya kutaka kupatiwa mafunzo ya KAIZEN, nina imani jitihada hizi zitazaa matunda kwa DART kuwa mtoaji wa huduma bora iliyo endelevu," alisema.

Zubeda Masoud akizungumza kwa niaba ya Katibu Mkuu (TAMISEMI), Prof. Riziki Shemdoe, aliwataka washiriki wa mafunzo hayo kutumia KAIZEN kuleta tija na mabadiliko kwenye mradi na maeneo yao ya kazi.

# WAJIKI wataka hatua rushwa ya ngono vyuoni

**Na Halfani Chusi**

TAASISI ya Wanawake katika Jitihada za Kimaendeleo (WAJIKI) inayojihusisha na utetezi wa haki za wanawake na watoto, imelaani vikali kitendo cha mmoja wa wahadhiri wa Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) kudaiwa kuomba rushwa ya ngono kwa wanafunzi wake.

Mkurugenzi Mtendaji wa taasisi hiyo, Janeth Mawinza, aliliambia Nipashe juzi kuwa kitendo kilichofanywa na mhadhiri huyo ni kibaya, cha kikatili na kinatakiwa kuchukuliwa hatua kali ili kuwa fundisho kwa wengine wenye tabia kama hiyo.

Alisema WAJIKI imekuwa ikipinga vitendo hivyo kupitia kampeni yake ya 'Safari Salama bila Rushwa ya Ngono kwa Wasichana na Wanafunzi Inawezekana'.

"Katika kampeni tumekuwa tukitoa elimu ya kupiga vita rushwa ya ngono kwa kushirikiana na vikundi vya madereva wa daladala, bajaj na bodaboda kwa kupita kijiwe kwa kijiwe na mitaani na kuanzisha klabu na kuendeleza klabu za jinsia na kupambana na rushwa ya ngono shuleni na kwenye mitaa mkoani Dar es Salaam, tunatoa elimu hiyo na kuwapa wasichana mbinu za kujiepusha na rushwa," alisema.

"Niseme tu kitendo kilichofanywa na mhadhiri huyo hakikubaliki, hivyo tunaomba mamlaka zinazohusika kuchuka hatua stahiki ili iwe funzo kwa wengine wenye tabia hizo.

"Pia ninapenda kukipongeza Chuo Kikuu cha Dodoma, binti kinara shujaa wa kupambana na rushwa ya ngono na wadau wote waliohusika kwa jitihada walizozifanya hadi kuhakikisha wamemnasa huyo aliyekuwa na nia ovu ya kufifisha ndoto za wanawake.

"Na sisi katika taasisi yetu huwa tuna usemi wetu usemao 'Mtaje, mwaibishe anayeomba rushwa ya ngono'. Na hicho ndicho kilichofanyika katika chuo hicho," alisifu.

Aliyataja madhara ya rushwa ya ngono yakijumuisha kuondoa utu, kupoteza nguvu kazi, kuathirika kisaikolojia, kushuka kwa uchumi wa familia na taifa, kifo, kupoteza malengo na kupata magonjwa ambukizi kama vile UKIMWI na Kaswende.

Miaka miwili iliyopita, Nipashe ilichapisha ripoti maalum iliyofichua kwa kina namna rushwa ya ngono inavyofanyika katika taasisi za elimu ya juu nchini, vikiwamo vyuo vikuu, ikuhusisha mwanafunzi kwa mhadhiri, mhadhiri kwa mhadhiri, mwanafunzi kwa mwanafunzi na mhadhiri au ofisa utawala chuoni dhidi ya mfanyakazi wa ngazi ya chini chuoni.

# Profesa apongeza ubunifu CBE

**Na Joseph Mwendapole**

WANAFUNZI wa Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) wamebuni vitu vingi ambavyo vinastahili kuingizwa kwenye maonyesho ya ubunifu wa teknolojia ikiwamo kuzima mitambo na vifaa vinavyotumia umeme kwa kutumia ujumbe wa simu ya mkononi.

Hayo yalisemwa jana chuoni huko na Mkuu wa Chuo hicho, Profesa Emmanuel Mjema, alipozungumza kwenye kongamano la wanataaluma wa chuo hicho kuelekea mahafali yanayotarajiwa kufanyika leo. Profesa Mjema alisema wanafunzi hao wamekuwa wakibuni vitu mbalimbali lakini inashangaza kuona chuo bado hakijatangaza ubunifu huo mkubwa ambao iwapo utaingizwa kwenye mashindano wanaweza kuibuka washindi.

Alisema CBE inafanya utafiti mbalimbali na ina maandiko yenye ubora wa hali ya juu ambayo yanasaidia katika ufundishaji lakini bado taarifa hizo hazijawafikia Watanzania wengi.

Profesa Mjema alisema katika mikutano ya kimataifa ya utafiti, CBE imekuwa ikishika nafasi ya kwanza kila mara kutokana na kuwa na maandiko na utafiti bora kuliko vyuo vingine.

"Mafanikio yote haya lazima tuyatangaze ili yatusaidie kujulikana duniani kwa sababu ile mikutano siyo ya Tanzania tu, kuna mataifa mengi yanahudhuria. Lazima tujivunie vitu vyetu na tuvionyeshe kunapokuwa na makongamano kama haya.

"Tunasikia watu wengi wanatusifia kwamba 'CBE you are the best' lakini sisi wenyewe kama bado tuna kaunyonge fulani hivi hatutambi kwa namna ambayo tunastahili kutamba kwa sababu tunastahili kutamba kutokana na mambo makubwa ambayo tumeshayafanya," alisema.

Mgeni rasmi kwenye kongamano hilo, Mkurugenzi wa Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara (TanTrade), Latifa Mohamed, alikipongeza chuo hicho kwa ubunifu mkubwa kwenye nyanja mbalimbali za kitaaluma hasa maendeleo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA). Akizungumza na waandishi wa habari mara baada ya kutembelea mabanda kwenye maonyesho chuoni hapo, Latifa alisema chuo hicho kimepiga hatua kubwa katika nyanja mbalimbali za kiteknolojia.

"Mimi nimesoma hapa kozi ya masoko, hivyo nina ushuhuda wa maendeleo makubwa yaliyofikiwa chuoni hapa. CBE imeona umuhimu wa kutumia teknolojia, ninatoa wito kwa Watanzania wote wawalete hapa kwa sababu hawa wana kozi zinazokwenda na wakati kwenye soko," alisifu.

Alisema kwenye maonyesho hayo, ameona ubunifu mbalimbali na alitoa wito kwa taasisi zinazodhamini wabinifu, kufika chuoni huko kuangalia vijana wa chuo hicho walivyo mahiri.

Alisema ameshangazwa na ubunifu wa vijana wanaosoma Teknolojia ya Habari na Mawasiliano kwa namna walivyobuni mfumo unaomwezesha mtu kuzima taa au kifaa chochote cha umeme kwa kutumia simu.

"Mfano unaweza kusahau kuzima mashine ya kufulia au kifaa chochote kinachotumia umeme lakini kupitia ubunifu huu wa vijana hawa unaweza kuzima kwa kutumia simu yako ya mkononi ukiwa popote pale, haya si maendeleo madogo, ni mambo makubwa sana," alisifu.




Meneja Biashara wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), Kemilembe Kafanabo, akizungumza katika uzinduzi wa vilainishi vya magari na mitambo kutoka kampuni ya Shell, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Vivo Energy yapania kuteka soko vilainishi

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Nishati ya Vivo Energy Tanzania, wauzaji na wasambazaji wa vilainishi vya kampuni ya Shell na Engen imerejesha nchini vilainishi hivyo na kuwataka Watanzania kuvitumia kwa usalama wa magari yao, ikitamba kuwa ni rafiki wa mazingira.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa vilainishi vya Shell, Meneja Biashara wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), Kemilembe Kafanabo, alipongeza jitihada za kampuni hiyo kwa juhudi zake za kusambaza bidhaa zenye ubora wa hali ya juu zenye manufaa kwa umma na jamii zikilenga sio tu kuongeza utendaji kazi wa magari na mitambo mingine lakini pia inalinda mazingira.

"Kama EWURA, tunatamani kuona vilainishi vinavyosambazwa nchini vinakidhi viwango vilivyowekwa. Kwa kufanya hivyo, tunalinda maslahi ya watumiaji na wananchi.

"Ili kuhakikisha bidhaa zinazosambazwa zinakidhi viwango vinavyotakiwa, EWURA inategemea kuanza kusajili vilainishi vyote vinavyosambazwa nchini. Hii ni pamoja na kuwasajili Vivo ambao wameidhinishwa kusambaza vilainishi vya Shell. hatua itakayopunguza usambazaji wa bidhaa ghushi nchini," alisema Kafanabo.

Alisema kuwa mamlaka hiyo iko tayari kufanya kazi bega kwa bega na waendeshaji wa kampuni hiyo ili kuboresha zaidi mazingira ya biashara ya vilainishi na kuhakikisha vitega uchumi vya jamii vinalindwa na watumiaji wanapata bidhaa zinazokidhi viwango vinavyotakiwa.

Mkurugenzi Mtendaji wa Vivo Energy Tanzania, Khady Sene, alibainisha kampuni hiyo imeamua kuingia mkataba wa kusambaza vilainishi vya Shell kutokana na umahiri wake kwenye uzalishaji wa vilainishi duniani.

Alisema kuwa teknolojia inayotumiwa na kampuni ya Shell ni ya kisasa inayokidhi matakwa ya kitaalamu, ikichangiwa na uwapo wake wa muda mrefu sokoni huku ikiaminiwa na kutumiwa na kampuni kubwa za magari na nyinginezo kubwa zinazohitaji huduma ya vilainishi.

Alisema ipo zaidi ya nchi 100 na Tanzania imefurahi kuwa kati ya nchi hizo na Vivo Energy Tanzania ndiyo wasambazaji pekee wa vilainishi hivyo nchini," alisema.

Mtaalamu wa Ufundi wa Vivo Energy, Fred Omondi alibainisha kuwa vilainishi vya Shell vitakavyokuwa vikiuzwa Tanzania ni hivyo hivyo vinavyouzwa nchi nyingine kubwa duniani kwa ubora na ufanisi wake.

"Tuna vilainishi vya aina tatu kama vile Shell Rimula kwa ajili ya mashine kubwa kubwa, Shell Helix kwa magari ya abiria na Shell Advance kwa ajili ya pikipiki," alifafanua Omondi.

# Tigo yaingia makubaliano kuinua huduma SACCOS

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya huduma za mawasiliano ya simu ya Tigo Tanzania imetia saini ya makubaliano na kampuni ya Norway inayofahamika kwa jina la Wakandi Group AS, ili kurahisisha huduma za kifedha kidigitali kupitia Tigo Pesa kwa SACCOS na taasisi ndogo za kifedha zilizosajiliwa.

Tigo pesa imeunganisha jukwaa lake la malipo na Wakandi's Credit Association Management System (CAMS) kwa ajili ya SACCOS na taasisi ndogo za fedha ili kudhibiti huduma zao za kifedha kwa ufanisi na kidigitali kwa urahisi na usalama zaidi.

Akizungumza katika tukio hilo, Ofisa Mkuu wa Huduma za Kifedha Tigo Pesa, Angelica Pesha, alisema: "SACCOS sasa zimekomaa zaidi na zinahitaji jukwaa la kisasa la usimamizi wa fedha. Hii ni kutokana na sababu kuwa wanahifadhi kiasi kikubwa cha fedha, wanatoa mikopo na kusimamia riba zake.

"Na ndio maana sisi kama Tigo Pesa tukachukua fursa hiyo kwa kushirikiana na Wakandi kuweka miamala yote ya SACCOS katika mfumo wa kidigitali kote nchini.

"Wakandi ina idadi kubwa ya wateja katika eneo lote la Afrika Mashariki, kwa hiyo ushirikiano huu unatupatia faida ya kiushindani kuwafikia wote waliotengwa katika huduma hizi za fedha za kidigitali hasa katika SACCOS.

"Kupitia mfumo huu, wanachama wataweza kutumia akaunti zao za Tigo Pesa kuchangia amana zao za SACCOS na kurejesha mikopo kupitia katika mfumo huohuo," alisema Pesha.

Mkurugenzi Mkuu wa Wakandi, Espen Kvelland, alisema SACCOS sasa zimekomaa zaidi na zinahitaji jukwaa la kisasa zaidi la usimamizi wa fedha. "Wakandi ina idadi kubwa ya wateja katika eneo lote la Afrika Mashariki, kwa hiyo ushirikiano huu unatupatia faida ya kiushindani kufikia watu waliotengwa kifedha nchini Tanzania na hasa katika nafasi za SACCOS. Wanachama wanaweza kutumia pochi zao za Tigo Pesa kuchangia amana zao za SACCOS na kurejesha mikopo kupitia chaneli hiyo hiyo, Tigo Pesa," Pesha ilisema.

Ili kupata huduma hiyo, SACCOS na taasisi ndogo za kifedha zinahitaji kusajiliwa na Wakandi Credit Association Management System (CAMS) kwa ajili ya wanachama wao, ambao ni wateja wa Tigo Pesa ili kukamilisha miamala yao bila matatizo kupitia menyu ya Tigo Pesa au kupitia Tigo Pesa App.





# Vijana waonywa mikopo halmashauri

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu, amewataka vijana wanaopata mikopo ya pikipiki inayotolewa na halmashauri kuitumia vizuri ili wajikwamue kiuchumi.

Ummy alisema hayo jana alipokuwa akizungumza kwenye hafla ya kukabidhi hundi ya mfano ya mkopo kwa vikundi vya wanawake, watu wenye ulemavu na vijana jijini hapa.

Waziri Ummy aliwataka vijana hao wanaokopeshwa vifaa hivyo vya usafiri, kuvitumia kwa malengo ya kuongeza mitaji ili waweze kurudisha kwa wakati na sio vinginevyo.

Baadhi ya vijana alisema waendesha bodaboda wanaopewa mikopo na halmashauri, badala ya kuzingatia sheria za barabarani wamekuwa wakiishia kuvunjika viungo vyao kutokana na matumizi mabaya, hali ambayo imekuwa ikisababisha kushindwa kurudisha mikopo hiyo kwa wakati.

"Ninyi vijana leo (jana) hii mnakabidhiwa mikopo yenu ya asilimia 10 ikiwamo ya fedha na vyombo vya usafiri bodaboda, guta na bajaji. Naomba mkaitunze na mkawe waangalifu katika uendeshaji wenu ili kurudisha mikopo hiyo kwa wakati,' alisema.

Naye Katibu Tawala wa Mkoa wa Dodoma, Fatuma Mganga, alisema vijana wanaongoza kuwa sugu wa kutorejesha mikopo, hivyo kuna haja ya kuweka sheria zitakazowabana ili warejeshe kwa wakati.

"Katika makundi yanayoongoza kwa usugu wa kutorejesha mikopo inayotolewa ya asilimia 10 na halmashauri zetu, ni vijana kutokuwa waaminifu katika kurejesha kwa wakati ili wengine wakopo fedha hizi," alisema.

Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma, Joseph Mafuru, alisema halmashauri hiyo ilianza kutenga na kutoa mikopo ya fedha zinazotokana na mapato ya ndani kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kuanzia mwaka wa fedha wa 2015/16.

Mafuru alisema kuanzia mwaka wa fedha 2015/16 hadi 2020/21, vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu vilivyonufaika na mikopo ya Halmashauri ya Jiji la Dodoma ni 1,546 vyenye wanachama 15,479 vikiwa na mzunguko wa Sh. bilioni 7.8.

Katika kipindi cha robo ya kuanzia 2021/22 jumla ya Sh. bilioni 1.39 zimekopeshwa kwa vikundi 48 vikiwamo vya wanawake 19 vijana 19 na watu wenye ulemavu 10. Kati ya fedha hizo, Sh. 238,514,365 ni mgawo wa robo ya kwanza na Sh. 100,535,635 ambazo zimevuka mwaka.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Ummy Mwalimu (katikati), akikata utepe kuzindua ugawaji wa pikipiki zilizotolewa na Halmashauri ya Jiji la Dodoma juzi, kwa ajili ya kuwakopesha vijana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

## Chifu ahamasisha sensa watu 2022

**Na PeterMkwavila,** DODOMA

CHIFU Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Henray Mtemi Mazengo, amewataka machifu kuisaidia serikali katika kuhamasisha jamii kujitokeza kwa wingi kushiriki sensa ya watu na makazi itakayo fanyika Agosti mwaka 2022.

Alitoa rai hiyo juzi alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu sensa hiyo itakayofanyika mwakani.

Chifu Mazengo alisema machifu wana wajibu mkubwa wa kuisaidia serikali ili kuhakikisha watu wanajitokeza kushiriki kuhesabiwa.

PIA aliwataka machifu wenzake kuzielimisha kaya ambazo zinaishi na watu wenye ulemavu kutowaficha ili wapate fursa hiyo ya kuhesabiwa kutokana na imani ya ushirikina iliyojengeka miongoni mwa jamii.

Chifu huyo alisema kuwa kitendo cha kuwaficha serikali itashindwa kupata takwimu sahihi ikiwa pamoja na kushindwa kupanga mkakati wake wa maendeleo kwa ajili ya Watanzania.

Hata hivyo, Chifu huyo aliishukuru serikali chini ya Rais Samia Suluhu Hassan, kwa kuwawezesha kutambuliwa uwapo wapo katika jamii na kuwashirikisha katika matukio mbalimbali ya kitaifa.

**PIA aliwataka machifu wenzake kuzielimisha kaya ambazo zinaishi na watu wenye ulemavu kutowaficha ili wapate fursa hiyo ya kuhesabiwa kutokana na imani ya ushirikina iliyojengeka miongoni mwa jamii.**

# Ujenzi wa ofisi osha waikuna kamati ya Bunge

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria imekagua jengo jipya la ofisi za Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA) lililopo jijini hapa na kueleza kuridhishwa na ubora wake.

Ukaguzi wa jengo hilo ulitanguliwa na kikao kifupi na wajumbe wa kamati hiyo kupokea taarifa ya ujenzi.

Akiwasilisha taarifa ya jengo hilo jana, Mtendaji Mkuu wa OSHA, Khadija Mwenda, alisema jengo hilo ni la ghorofa tano na kwamba limegharimu Sh. bilioni 4.8, kiwango ambacho ni cha chini ya makadirio ya awali ya bilioni 6.56 pamoja na kodi.

"Mradi huu wa jengo la ofisi za OSHA Dodoma tumeutekeleza kwa muda wa miezi nane kuanzia Agosti 22, 2020 hadi Aprili 21, 2021.

"Kutokana na kutekeleza mradi huu kwa wakati pamoja na usimamizi mzuri uliofanywa na OSHA, Mkandarasi na Mshauri Mwelekezi, tumefanikiwa kuokoa zaidi ya Sh.milioni 650," alisema Mwenda.

Alisema pamoja na kujenga jengo hilo kwa muda mfupi na kutumia gharama ndogo, mradi huo umetekelezwa kwa kuzingatia sheria na taratibu zote za ujenzi, viwango stahiki vya ubora, usalama pamoja na mahitaji ya watu wenye ulemavu.

Akizungumza kwa niaba ya wanakamati hiyo baada ya kutembelea maeneo tofauti ya ofisi hiyo, Emmanuel Mwakasaka alisema wamefarijika baada ya kuona mradi huo umetekelezwa kwa kuzingatia taratibu zote za ujenzi na viwango stahiki.

"Tumewahi kukagua majengo mengi sana kama kamati lakini mimi niseme kwa mara yangu ya kwanza tumeweza kukagua jengo ambalo si tu wanakamati wameridhika nalo bali ni jengo ambalo kamati yetu haijaona dosari. Hivyo, nimpongeze Mtendaji Mkuu wa OSHA," alisema.

Ng'wasi Kamani, mjumbe wa kamati hiyo, alisema moja ya majukumu ya kamati hiyo ni kusimamia taasisi zilizoko chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, ikiwamo OSHA.

"Tumepata bahati ya kutembelea jengo hili la OSHA. Tumeona limejengwa ndani na muda mfupi hivyo tulitarajiwa kuambiwa kwamba limejengwa kwa gharama kubwa lakini tumefurahi kusikia kwamba ujenzi umekamilika kwa bajeti ambayo ni chini ya makadirio ya awali lakini pia limejengwa kwa viwango stahiki." alisema

Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Masuala ya Watu Wenye Ulemavu, Ummy Ndelianange, alisema anajivunia mafanikio yaliyopatikana katika mradi huo ikiwamo ujenzi kufanyika katika viwango stahiki vya ubora pamoja na kutumia bajeti kidogo na hivyo kuokoa zaidi ya Sh. milioni 650.

Jengo hilo limejengwa na kampuni ya ujenzi ya kizawa ya Estim Construction Co. Ltd chini ya Mshauri Mwelekezi Chuo Kikuu cha Ardhi na umetekelezwa kwa muda wa miezi minane tu. Katika kipindi hicho chote, ajira 682 zikiwemo za watu wenye ulemavu zilitengenezwa na unatarajia kutengeneza zaidi ya ajira 1,500 baada ya jengo hilo kuanza kutumika.





# Ukarabati jengo la kihistoria waiva

**Na Rahma Suleiman**, ZANZIBAR

WAZIRI wa Utalii na Mambo ya Kale, Lela Muhamed Mussa, amesema jengo la makumbusho ya kale la Beit-al-Jaib linatarajiwa kufanyiwa ukarabati mkubwa mapema mwakani.

Waziri huyo aliyasema hayo jana alipotembelea jengo hilo akifuatana na Balozi Mdogo wa Oman aliyepo Zanzibar, Said Salum.

Alisema mipango ya ukarabati wa jengo hilo tayari imekamilika na utafanyika Februari mwakani chini ya ufadhili wa serikali wa Oman ambayo imekubali kutoa Dola za Kimarekani milioni 5.9.

Lela alisema ukarabati wa jengo hilo utafanyika chini ya usimamizi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) ambalo ndilo linaloshughulikia majengo yote ya kale yaliyoko chini ya uhifadhi wa urithi wa kimataifa.

Alisema ukarabati huo lengo lake kwa asilimia kubwa ni kurudisha uhalisia wa jengo lililoporomoka na kuwapo kwa haiba ya urithi wa kimataifa wa mambo ya kale.

"Napenda kuwajulisha wananchi na wadau wa sekta ya utalii kwamba ukarabati mkubwa wa jengo la kumbukumbu ya kale la Beit-al-Jaib unatarajiwa kufanyika mapema mwakani na maandalizi yote yamekamilika," alisema.

Naye Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Fatma Mbarouk, alisema zabuni ya ujenzi wa ukarabati wa jengo hilo inatarajiwa kuitishwa mwezi huu.

"Tunatarajia kutangaza zabuni ya mjenzi atakayefanya ukarabati mkubwa wa jengo la Beit-al-Jaib na kulirudisha katika uhalisi wa awali baada ya kuporomoka baadhi ya sehemu zake ikiwemo sura ya mbele ya jingo," alisema.

Balozi Salum kwa upande wake alisema wamejipanga kikamilifu kulifanyia ukarabati jengo hilo ambalo limebeba historia kubwa ya Zanzibar pamoja na haiba ya mji wa Zanzibar ya majengo ya kale.

"Serikali ya Oman ipo tayari kulifanyia ukarabati mkubwa jengo la Beit-al-Jaib ambalo limeporomoka na tayari mipango yote imekamilika ikiwamo kutenga fedha kwa ajili ya mradi huo," alisema.

Ukarabati wa jengo hilo ni sehemu ya mikakati ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuimarisha sekta ya utalii ambayo kwa asilimia 50 huchangia pato la taifa na fedha za kigeni.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Alhaj Dk. Hussein Ali Mwinyi, akizungumza na waumini wa Dini ya Kiislamu, baada ya Sala ya Ijumaa katika Masjid Fatma Kibanda Hatari, Wilaya ya Mjini, Mkoa wa Mjini Magharibi, jana. **PICHA: IKULU**

# Rais awakumbusha watendaji kuwajibika

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amewataka viongozi na watendaji wa wizara na idara za serikali kutekeleza wajibu wao katika kusimamia mifumo ya ukusanyaji na matumizi ya fedha za Serikali.

Pia amebainisha kuwa serikali haitegemei ripoti ijayo ya June, 2022 kusheheni lundo la dosari.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo juzi Ikulu Zanzibar baada ya kupokea taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali (CAG).

Alisema viongozi na watendaji wana wajibu wa kutekeleza majukumu yao ipasavyo katika kusimamia mifumo ya ukusanyaji na matumizi ya fedha, huku akionya endapo ripoti ijayo itafanana na iliowasilishwa kwake, itamaanisha bado viongozi na watendaji hao hawajachukua hatua zinazostahili.

Suala la bajeti, alisema ni muhimu katika kutekeleza mipango ya serikali na kusisitiza kuwa hilo si jukumu la CAG pekee bali ni la viongozi na watendaji wote.

Alisema kila mmoja ana wajibu wa kurekebisha hali hiyo na kusema malalamiko mengine yanayotolewa na watendaji hayazingatii wajibu walionao katika kusimamia makusanyo na matumizi ya fedha za umma.

Kwa mujibu wa Dk. Mwinyi, ripoti iliyowasilishwa imebainisha kuwa fedha nyingi zinazopaswa kuingia serikalini haziingii.

Dk. Mwinyi alikumbusha umuhimu wa watendaji hao kutembelea taasisi zao ili kuhakikisha zinatekeleza wajibu wao, ikiwamo wa ukusanyaji wa mapato na matumizi yake huku akisisitiza kwamba mfumo wa kutoa taarifa za CAG hadharani utaendea ili wananchi kupata taarifa.

Naye CAG Dk. Othman Abass Ali akiwasilisha mwendelezo wa ripoti ya ukaguzi wa mfumo wa usimamizi wa fedha, ikiwa ni maagizo yake ya kurejewa ukaguzi huo, alisema taarifa za ukaguzi huo ni wa miaka mitano.

Alisema lengo ni kuhakikisha kunakuwapo udhibiti mzuri wa fedha na kubainisha dosari kadhaa zilizobainika, ikiwamo ya taarifa za hesabu za hazina kutokuunganishwa na mfumo kwa maana ya kuwa hesabu hizo zimerikodiwa kwa mkono 'manual' katika Benki Kuu ya Tanzania (BoT) pamoja na Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ).

Kwa mujibu wa CAG, athari kubwa za matumizi ya mfumo huo 'manual' ni kutoa fursa ya kufanyika matumizi yasio rasmi au matumizi holela.

Alisema changamoto nyingine ni ya kuwepo kwa hesabu za wizara, idara na wakala wa serikali ambazo hazikuunganishwa na mfumo, hivyo kukusanya mapato na kurekodi kwa njia ya mkono.

Akitoa mfano wa mwaka 2019, alisema katika vitabu vya taasisi vilionyesha serikali ilikuwa na bakaa ya Sh. Bilioni 1.2 lakini benki hakukuwa na fedha kabisa.

# Bil. 51/- kuwezesha wananchi kiuchumi

**Na Rahma Suleiman**, ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imetenga Sh. 50,636,032,910 ambazo zimetolewa na Shirika la Fedha Duniani (IMF) kwa ajili ya kuwawezesha wananchi kiuchumi wakiwamo wajasiriamali.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Mudrik Ramadhan Soraga, alisema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake, Mwanakwerekwe, kuhusu fedha zilizotolewa na IMF katika kupambana na ugonjwa wa corona.

Alisema uwezeshaji huo unatarajiwa kuwanufaisha wajasiriamali na wafanyabiashara kutoka 85,850 Unguja na Pemba.

"Fedha hizi zitawanufaisha wajasiriamali na wafanyabiashara wote wakiwamo wanawake, vijana, watu wenye ulemavu, wajane, vijana wanaoacha dawa za kulevya na wananchi wote wanaojishughulisha na biashara mbalimbali,"alisema.

Waziri huyo alisema wajasiriamali 2,906 wenye viwanda wametengewa Sh. 4,056,000,000, waendesha bodaboda kila mkoa watapatiwa pikipiki 50 ambapo eneo hilo limetengewa Sh 6,72,000,000 na wakulima na wafugaji 8,444 wametengewa Sh. 6,760,080,000.

Alisema serikali kupitia wizara yake kwa kushirikiana na taasisi za fedha, inaweka utaratibu na miongozo mizuri ya wananchi kufaidika na kunufaika na fedha hizo.

Soraga alisema vigezo hivyo ni pamoja na kuwa na biashara au kuwa na kikundi kinachotambulika rasmi na kupata usajili ambapo kitatumika kama dhamana ya mkopo utakaochukuliwa na uwezo wa usimamizi na matumizi ya fedha hizo.

Pia alisema Serikali imedhamiria kuimarisha uzalishaji wa asali kwa sababu bidhaa hiyo ina soko kubwa ndani na nje ya nchi ili kuimarisha ufugaji wa nyuki.

Alisema fedha hizo zitakazotolewa zitaondoa ukosefu wa mitaji ya kuimarisha biashara za wajasiriamali.

Waziri aliwataka wajasiriamali kutoogopa bali wajitokeze kwa wingi kwenda kuchukua mikopo hiyo ili kuimarisha bidhaa zao na uzalishaji wakati serikali inaendelea kuimarisha upatikanaji wa masoko ya bidhaa mbalimbali wanazozalisha.



**POLE TRAVIS MWOMBE MUNGU ATAKUSAIDIA** Uk.14

Nipashe MWANGA WA JAMII
BT BURUDANI TELE
JUMAMOSI NOVEMBA 13, 2021



## WACHA DIAMOND ATUMIE

# Wengine watahesabu vidole

HIVI karibuni msanii nyota wa muziki nchini, Diamond Platnumz, akiwa Marekani kwenye ziara zake za muziki, alifanya vitu ambavyo vimekuwa gumzo.

Wakati baadhi ya vijana wanapata pesa kwa jasho, lakini anazimaliza kwa kunywea pombe na anasa zisizo na kichwa wala miguu, yeye anajua kutumia pesa kwa kujiburudisha mwenyewe, jinsi roho yake inapenda. Siyo kumburudisha mwingine.

Jamaa anajua kuzitumia pesa zake anazozikeshea na kuzitolea jasho. Kwanza kabisa aliingia kwenye duka maarufu la 'Watch Empire' huko Los Angeles na kununua saa aina ya 'Rolex,' ambayo inakadiriwa kuwa na thamani ya zaidi ya Sh. milioni 60 kwa pesa za Kitanzania.

Kama vile haitoshi, Diamond akatumia kiasi cha pesa kinachokadiriwa kuwa ya zaidi ya mlioni mia moja kununua mkufu wa dhahabu wenye kidani chenye vito vya almasi .

Mwenyewe hata hakuficha. Baada ya ununuzi huo, akaandika kwenye mtandao wake wa kijamii wa instagram

"Milioni 69 kwa saa, dhahabu na almasi acheni kuvaa mkufu bandia wavulana wadogo, kuna saratani. Dola 48,000 sawa na 111,360,000, naondokaje sasa? Ameandika Diamond.

Hapo ina maana Mondi katumia kiasi cha milioni 111.4 kununua saa na cheni yenye vito ya dhahabu na kidani cha almasi.

Habari hii imekuwa gumzo kwa Wabongo kwenye mitandao ya kijamii na hata mitaani na vijiweni.

Vijana wa kiume, wameonekana kushangazwa sana na kiasi hicho cha pesa alichotumia kununua mapambo pekee.

Ndiyo, wanafahamu kuwa msanii huyo ni tajiri na ana pesa, lakini hawakudhani kama anaweza kutumia pesa zote hizo kununua saa na mkufu tu.

Wengine wanasema wangezipata pesa hizo wangekuwa na nyumba mbili za milioni 50 tu kila moja.

Ni pesa ambayo unaweza kujenga nyumba yako nzuri tu na kukuepusha na kadhia ya kupanga, kila siku kulalamikiana na mama au baba mwenye nyumba.

Baadhi wanasema kama wao wangezipata hizo pesa ambazo Mondi kanunua mkufu na saa kwa muda mfupi, wangeanzisha biashara.

BASI SAWA

## Babalevo wazo lako sawa, lakini...

WAZO la mwanamuziki wa kizazi kipya Babalevo, ambaye hivi karibuni alishauri serikali na kampuni kuwakutanisha mastaa wapinzani Diamond na Alikiba, ili ijulikane nani mbabe, limeibua mjadala mkali kwa wapenzi na mashabiki wa muziki nchini.

Babalevo alisema wasanii hao wametambiana kwa muda mrefu, hivyo ni muda wa kutengeneza pesa kwa kupambana jukwaani kwa kwenda mkoa kwa mkoa.

Baadhi ya watu wamesema wazo la Babalevo halina mashiko kwa sababu anajua wasanii hao ni vigumu kutumbuiza jukwaa moja na kibaya zaidi hata viongozi wa ngazi ya juu waliojitokeza kuwaweka sawa hawakufanikiwa.



## Hasira zingine bhana!

NI hasira tu! Pengine ndivyo ilivyokuwa kwa mwanamuziki wa Bongo Fleva, Harmonize, baada ya kuchukua hatua kali ya kumwondoa katika orodha ya wafuasi wake bosi wake wa zamani Diamond Platnumz.

Katika ukurasa wa Harmonize, amechukua hatua hiyo bila kutoa sababu, lakini kwa upande wa Diamond, ameonekana kuchukulia jambo hilo kwa umakini kwani bado hajamfuta katika orodha ya wafuasi wake.

Mastaa hao wapo katika bifu kali baada ya Harmonize kuamua kujitoa katika lebo ya WCB na kuibuka ushindani mkali kati ya wanamuziki hao wawili ambao muziki na sauti zao zinalingana.





## Shilole usiseme tu, mazoezi yanakuhusu

SASA Shilole kaamua, kwani anataka kwenda gym kupunguza ubonge aliokuwa nao.

Kwenye Siku ya Mwananchi iliyoandaliwa na klabu ya Yanga, Agosti mwaka huu, katika uwanja wa Benjamin Mkapa, wengi walishangazwa na mwili wa msanii huyo kuwa kibonge.

Baadhi ya watu walimshauri kupunguza unene, maana ulikuwa umezidi.

Shilole ametoa taarifa kupitia ukurasa wake wa Instagram, akiambatanisha na picha yake ya zamani kabla hajakuwa na mwili mkubwa kisha akaandika.

"Je, umemjua huyo binti hapo, kama ndio basi kakubali kurudi gym na anataka traina wa kumfata kwake malipo sio shida, kikubwa mazoezi yawe standard sio kukomoana maana walimu wengine khaaaaa"





## Ali Kiba wakati mwingine busara zinatoa jibu sahihi

MWANAMUZIKI nyota wa kizazi kipya, Ali Kiba, ameonekana akutumia busara kumjibu msanii mwenzake Niki Mbishi, ambaye alimnanga kwa kusema si mzuri kuimba mistari ya wimbo.

Ali Kiba amesema anakubaliana na mawazo ya Niki Mbishi, kwamba yeye anaimba kwa kuungaunga, lakini akatilia wasiwasiwasi uelewa wake na uwezo wake wa kufikiria mambo magumu.

Hata hivyo amewaomba mashabiki wake kumvumilia rapa huyo na kwamba yote aliyosema ni maoni yake na yeye kama mhusika mkuu anayachukua na kuyafanyia kazi.

## Kufuli Love, Nandy, Zuchu pambe

**Na Adam Fungamwango**

MWEZI Novemba umeingia kwa kishindo, baada ya wasanii mbalimbali kutoa ngoma zao ambazo zimeanza kutingisha kwenye mitandao ya kijamii, radio na televisheni.

Baadhi ya wasanii maarufu hawakutaka mwezi huu uishe hivi hivi, ni kama vile wameshindana kutoa pini kali na sasa zimekuwa gumzo.

Kuanzia Novemba 5, wakaanza kutupia moja baada ya nyingine, wengine wakitoa albamu zao kabisa.

Leo tunaangalia baadhi ya madude yaliyotolewa mwezi huu wa Novemba.

**JELA-RUBY**

Huu siyo wimbo wa mapenzi wala nini. Ni kwamba Ruby ameongea kwa lugha ya picha. Siyo jela unayoijua wewe ile ya kwenda kukaa huku ukilindwa na askari magereza. Jela anayoizungumzia hapa ni jela ya pesa. Mtu akikosa pesa, kila shida zitamuandama. Mtoto wake ataumwa, ndugu zake watapata matatizo mbalimbali, lakini anashindwa kufanya chochote kwa sababu tu hana pesa za kutatua matatizo yanayomkabili. Ngoma hii imetoka Novemba 5 na sasa inabamba kinoma.

**KUFULI-NANDY FT MARIO**

Huu ni wimbo wa mapenzi, ambapo mwanamke anamwambia mpenzi wake asimchanganye na mwanawake mwengine ambayo hawana hadhi naye. Kipande hicho anaimba Nandy, anamwambia yeye ana hadhi ya juu, hivyo akigundua kuwa akitoka kwake, halafu anawataka na wanawake wengine wa mtaani 'viswaswadu', atamkasirisha.

Mario aliyeimba kipande hicho anamjibu kuwa hatofanya hivyo kwa sababu anampenda, lakini akampa angalizo kuwa ampe mapenzi ambayo yatamfanya asiwatamani wanawake wengine. Umefyatuliwa Novemba 6.

**NAMKUMBUKA-BARAKAH THE PRINCE**

Siku mbili baadaye, yaani Novemba 8, msanii, Barakah the Prince akatoa pini yake aliyoiita 'Namkumbuka'.

Ni wimbo wa mapenzi ambayo ni yale yale ya siku zote, mtu anapojikuta mpweke mpenzi wake anapoondoka.

Kuna wakati wapenzi hugombana wanapokuwa pamoja, lakini mmoja akiondoka kwa kukorofishana tu, anajikuta mpweke, kiasi kwamba hata yale anayokufanyia unaona ni afadhali kuliko unavyojikia mpweke alivyoondoka.

**BAILA-RAYVANNY**

Rayvanny mwezi huu wa Novemba yeye akatoka na kitu chake chenye jina la 'Baila'.

Anamwambia mpenzi wake jinsi anavyompenda, anaweza kufanya hata vitu ambavyo haviwezekani. Anaweza kumfuata hata Zanzibar kwa kutumia usafiri wa Bajaj. Ngoma hii imeitoa Novemba 9 na tayari mzigo uko hewani.

**FOR YOU LOVE-MBOSSO FT ZUCHU**

Mbosso yeye akatoa ngoma moja aliyoipa jina la 'For You Love', Novemba 10. Amemshirikisha msanii wa kike Zuchu.

Ni wimbo wa mapenzi, ambapo wanaonekana wako kwenye mahaba mazito, kila mtu akimsifia mwenziwe, akieleza jinsi gani anavyompenda. Haina tofauti na zile filamu za kihindi zenye maneno na matendo wa mahaba.


NANDY




## Chozi la aibu; Mali iliyojaa damu

**Na Adam Fungamwango**

CHOZI la aibu ni filamu inayomzungumzia mama mmoja aliyeachiwa mali na watoto na marehemu mumewe na mke mwenzake. Lakini akaona mali ni kitu chenye thamani zaidi kuliko watoto. Walikuwa ni watoto wa mke mwenzake. Tena wote wawili aliwaua yeye mwenyewe ili apate mali hizo, lakini waswahili wanasema 'muda ni mwalimu mzuri.'

Ni filamu yenye mafundisho mazuri kwa jamii, kwani wapo watu ambao hufikiria mali zaidi kuliko utu. Wanaweza hata kuua ili kupata mali. Mtu anaweza kumuua mumewe, mkewe, baba au mama ili tu arithi mali. Haya yapo sana kwenye jamii.

Imechezwa na Aisha Hamisi kama Suzan, Salma Maneno kama Salma, Juma Ally aliyecheza kama Mbayu, Edward Sanga yeye alivaa uhusika wa Shiko, Kasele Ramadhani kama Shaka.

Inaanza kuonyesha Shaka anaumwa. Yuko hoi bin taaban. Anatoa usia kwa rafiki yake Shiko, kuwa akifa mali zake zigawanywe kwa mkewe mkubwa ambaye ana watoto wawili na pia ni mjamzito. Pia mkewe mdogo ambaye hajabahatika kupata mtoto naye pia apate mali yake. Baada ya hapo akafariki dunia. Hata hivyo yote hayo aliyafanya mke mdogo. Alimuua mumewe kwa madawa ya kienyeji ili apate mali. Baada ya kifo cha shaka, zamu ikawa kwa mke mwenzake. Huyu hakuuawa kwa madawa. Alijifanya anampeleka kliniki, walipofika njiani porini, alimpiga na gongo kichwani na tumboni, akafa pale pale. Suzan akabaki na watoto wawili wa mke mwenzake, Mbayu na Salma. Akaanza kuwatesa. Wakateseka hadi majirani wakaja juu. Hilo halikuwa tatizo kwa Suzan, mwisho akawafukuza kabisa nyumbani.

Katika kutembeatembea wakachukuliwa na baba mmoja, akawapeleka kwa mkewe ili awalee.

Mzee aliwalea kwa mapenzi mema na mkewe hadi walipokuwa wakubwa, akaenda mjini kutafuta maisha. Maisha yaliwakubali. Hawakusahau kwao. Walirejea na kumkuta mama yao aliyewalea amefariki, lakini baba yao yupo. Walirudisha fadhila kwa mzee yule. Wakaamua kupitia kwa mama yao wa kambo aliyewanyanyasa na kuwafukuza. Walimkuta hoi. Anaumwa hana hata wa kumtibia. Pia amezeeka sana. Mbayu aliamua kumchukua kumpeleka mjini ili apate matibabu anayostahili. Salma alikataa kwa sababu ndiye aliyemnyanyasa. Mbayu alimpeleka mjini, akamtibia na kupona. Yeye akasema halipi kisasi kwa yote yaliyotokea. Salma bado alikuwa na kinyongo. Hata hivyo mama alianguka chini ya miguu yake. Akaomba msamaha na kudai kuwa ujana na tamaa ya mali ndiyo vilimfanya awe vile. Hatimaye Salma anamsamehe.



# Kanye, Kim mwendo wa kisasi

MWENDO wa kisasi! Unaweza kusema hivyo baada ya Kanye West na aliyekuwa mkewe, Kim Kardashian, kuonekana wakirushana roho kwa kuonekana wakiwa na wapenzi wao wapya.

Rapa Kanye West, amelipiza kisasi kwa Kim ambaye hivi karibuni alionekana akiwa na kijana mdogo wa miaka 18, Pede Davidson, na yeye ameonekana akiwa na mwanamitindo Vinetria.

Kulingana na mtandao wa PageSix, Kanye na Vinetria wameonekana wakiwa pamoja mwishoni mwa wiki wakati wakifuatilia mpira wa kikapu katika mji wa Minneapolis.



## Jennifer Lopez usimpagawishe Ben kihivyo

SASA ni mapenzi motomoto kila mahali kwa mastaa Jennifer Lopez and Ben Affleck, na imefikia wakati wawili hao hawajali wako wapi pale wanapotaka kuonyesha wamelewa kimahaba.

Wapenzi hao wa siku nyingi ambao waliachana na kurudiana hivi karibuni, wamejikuta wakipeana mabusu motomoto katika uwanja wa ndege wa Los Angeles, kabla ya J Lo kupanda ndege binafsi na kwenda nje ya mji huo.


Ben ambaye ni msanii maarufu wa filamu aliamua kurudisha mapenzi kwa mkewe huyo wa zamani na kuwashangaza mashabiki wao kutokana na jinsi wanavyoonyesha hadharani mapenzi yao.

## Baba Ijesha mengi yafichuka

OFISA wa polisi, ASP Wahab Kareem , ameiambia mahakama kwamba mwigizaji nyota wa Nollywood, Olanrewaju James maarufu kama “Baba Ijesha” anafanyiwa uchunguzi mwingine wa unyanyasaji wa kingono na mtoto wa kike.

“Tulimhoji yeye na mshtakiwa nyuma ya kaunta, alikanusha vikali shtaka hilo, lakini msichana huyo alisema tukio hilo lilitokea eneo la Agah, Ikorodu, tukamwambia mwakilishi wa mshtakiwa amfuate hadi nyumbani kwake, tukakutana na mwenye nyumba na kutuonyesha ghorofa ambalo Baba Ijesha alikuwa anakaa’.” Amesema shahidi huyo.



## Pole Travis mwombe Mungu atakusaidia

POLISI wanaendelea kuchunguza tukio la vurugu lililosababisha watu wanane kufariki dunia katika tamasha la muziki la rapa Travis Scott, lililofanyika mjini Houston, nchini Marekani.

Tukio hilo limetokea Ijumaa ya wiki iliyopita, baada ya mashabiki kukanyagana baada ya kuibuka vurugu karibu na jukwaa.

Taarifa kutoka kikosi cha uokoaji, imeeleza idadi hiyo ndiyo iliyothibitishwa lakini kuna watu wamejeruhiwa vibaya na kukimbizwa Hospitali na hivyo inaweza kuongezeka.

## Faith kakwambia nani mwanamke ukawa mbabe?

MWANAMUZIKI wa Marekani, Faith Evans, na mume wake Stevie J, wamekubaliana kupeana talaka na kuhitimisha ndoa yao ya miaka minne.

Kwa mujibu wa mtandao wa TMZ, Stevie J amefungua faili la talaka baada ya mkewe huyo kushinda tuzo hivi karibuni.

Taarifa zinaeleza maombi hayo ya talaka yamefunguliwa Jumatatu ya wiki hii, katika mahakama ya juu kwenye jimbo la Los Angeles.

Imeelezwa katika maisha yao ya ndoa, Faith alikamatwa na kuwekwa mahabusu mwaka 2018 kwa tuhuma ya unyanyasaji na mgogoro wao uliendelea kukua hadi kufikia hatua ya kuvunja ndoa yao.



MAKALA

## BURIANI

# Dk. Weggoro; Shujaa mzalendo aliyeongoza nchi nyuma ya pazia

Na Derek Murusuri

TANZANIA imebarikiwa na Mungu kuwa Taifa lenye watu werevu, wenye vipaji na wazalendo wa kweli. Katika watu hao, Dk. Nyamajeje Calleb Weggoro, hawezi kuachwa nyuma katika orodha hiyo.

Aidha, viongozi wazuri na makini kote duniani, huchagua wasaidizi wenye uwezo mkubwa na wenye vipaji ili kusaidia kushauri namna njema ya kulileta taifa maendeleo.

Miongoni mwa wasaidizi mahiri na wenye uwezo mkubwa wa kusuka mikakati yenye matokeo makubwa katika Tanzania, Dk. Nyamajeje Calleb Weggoro hawezi kufutika katika kumbukumbu ya mashujaa hao.

Nilipomwona Rais wa Awamu ya Nne, Dk Jakaya Kikwete, alipokuja kuhani msiba nyumbani kwa wanafamilia wa marehemu, Bunju Novemba 11, 2021, nikakumbuka mbali.

Kama mameneja wenye mafanikio makubwa duniani walivyo, Kikwete alikuwa na uwezo mkubwa wa kubaini vipaji ndiyo hakuchelewa kumteua Dk. Weggoro kuwa msaidizi wake katika masuala ya utengamano na uchumi.

Nchini Tanzania, endapo kuna mwananchi mmoja mwenye kuijua Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) nje ndani, basi hakuna mwingine kwenye nambari moja, zaidi ya Dk. Weggoro.

Alikuwa mmoja wa Watanzania wawili, mwingine akiwa Balozi Fulgence Kazaura, aliyefariki dunia akiwa Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM).

Ni Watanzania hawa pamoja na wenzao kutoka Kenya na Uganda, waliotumia maarifa mengi kuhakikisha viongozi wa nchi hizi tatu wanaweka nyuma maslahi madogo ya mataifa yao na kuweka mbele maslahi mapana ya jumuiya.

"Haikuwa kazi rahisi," anakiri Dk. Weggoro katika mazungumzo yetu katika 'lounge' ya Safari Hotel, jijini Arusha.

Dk. Weggoro alikuwa katika Kamisheni ya Kudumu ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki, yaani 'Permanent Tripartite Commission for East African Cooperation'. Makubaliano yake yalitiwa saini na viongozi wa mataifa haya ya Afrika Mashariki, Kampala, Uganda 30 Novemba 30, 1993.

Machi 14, 1996, ilizinduliwa sekretarieti yake Arusha na Dk. Weggoro akiwa mjumbe kutoka Tanzania.

Alifanya kazi hiyo ya kihistoria ambayo iliisuka upya EAC na kuipa sura ya leo. Dk. Weggoro alipenda jumuiya ifanikiwe zaidi ya sasa. Aliienzi tunu ya umoja. Aliishi pia.

Jukumu hilo lilimfanya awe akivinjari katika Ikulu za mataifa haya matatu ya Afrika Mashariki. Viongozi wa mataifa hayo walimpa heshima kubwa kutokana na matokeo ya kazi yake pamoja na heshima aliyowajengea mbele ya wananchi.



**HAYUPO TENA**

Dk. Weggoro hayuko nasi tena. Amefumba macho na hawezi kuyafumbua tena. Kazi zake zingali zinaishi.

"Habari? Niko Pretoria kwa matibabu. Wiki sasa. Napambana," ulikuwa ujumbe mfupi wa WhatsApp alioniandikia Septemba 24, 2021.

Hakika, Dk. Weggoro alikuwa mpambanaji. Hakuwa mtu wa kukata tamaa kwa wepesi. Alikuwa mwepesi wa kutafuta mikakati ya ziada hadi kupata matokeo.

Ndiyo maana Kikwete alimchukua kuwa msaidizi wake katika Ofisini ya Rais ili amshauri katika masuala ya utangamano wa kikanda na uchumi mwaka 2013. Mwaka 2015, alipoingia Rais wa Awamu ya Tano, Dk. John Magufuli, ulikuwa wakati wa Dk. Weggoro kustaafu utumishi wa umma.

Alipokwenda kumjulisha bosi wake, Dk. Magufuli alimkatalia. "Uondoke hapa Ikulu, mimi anisaidie nani, kapige kazi," aliambiwa. Hakuna kiongozi aliyetaka kuiachia lulu hii ambayo imeitwa na Muumba wake.

Mwaka 2016, alipoteuliwa kuwa Mkurugenzi wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), akiiwakilisha benki hiyo katika mataifa manane ya Afrika, alifanya kazi kubwa ya kukuza uchumi wa mataifa hayo. Alisimamia mataifa ya Tanzania, Kenya, Uganda, Ethiopia, Rwanda, Eritrea, Shelisheli na Sudan Kusini.

Alikuwa kama kejeri kwa kijita ni kindege kidogo kijanja ambacho hakisahau kwao. Tanzania ilifaidika na inaendelea kufaidika na ufadhili wa miradi mbalimbali ya maendeleo kutoka AfDB. Hii ni kutokana na kazi nzuri aliyoifanya Dk. Weggoro.

Uhusiano baina ya Tanzania na AfDB uliimarika. Ni yeye aliyehakikisha AfDB inatoa fedha za ujenzi wa kiwanja cha ndege cha Msalato na mambo mengine mengi. Tanzania imempoteza mpiganaji wake mahiri, mwenye uwezo mkubwa wa kufikiri.

Siku moja, akiwa anahojiwa na kituo cha TV ya kiganjani ya Arusha, alikielezea kitabu changu, "Making Africa World's Largest Economy'" kuliko mimi mwenyewe niliyekiandika.

Alidhamini nakala 70 zikasambazwe bure katika shule za sekondari za Mkoa wa Mara kama sehemu ya mchango wa kuhamasisha maendeleo ya fikra. Alinieleleza nivikabidhi vitabu hivyo kwa Mkuu wa Mkoa wa wakati huo, Adam Kighoma Malima.

Alibeba ajenda ya maendeleo moyoni mwake. Aliheshimu kipaji, bila kujali umri au haiba ya mtu.

Alibeba vipaji vingi. Alikuwa msomi wa PhD kutoka Ujerumani akiwa mahiri katika uongozi, uchumi, fedha, mipango, menejimenti, uhandisi wa viwanda, usimamizi wa miradi na ujenzi wa uwezo kwa watu na wafanyakazi. Huenda ndiyo maana wanahisa wa Benki ya Afrika (BOA) walimteua kuwa Mwenyekiti wa Bodi wa Benki hiyo, ambayo tayari alishaanza mipango ya kuifanyia mageuzi, kuongeza matawi na bidhaa.

Nilibaini vipaji vingi vya Dk. Weggoro, Mei, 2020, pale tulipokaa zaidi ya saa tatu (3) tukinywa chai. Nikibaini kuwa Dk. Weggoro hakuwa binadamu wa kawaida. Ni siku hiyo nilifahamu kwa nini viongozi wengi walipenda kufanya naye kazi.

Dk. Weggoro alikuwa binadamu aliyekuwa rafiki wa wafalme lakini kamwe hakumdharau binadamu wa chini.

"Nakuja Dar, tuonane tukale ugali na kibambala cha sato hapo kwa Daudi," alisema akimaanisha Break Point.

**TUMEMPOTEZA**

Alikuwa karibu sana na watu wa kada zote. Alikuwa taasisi. Alikuwa shule. Alitafuta, akatunza na kutumia maarifa mengi kwa maendeleo ya Tanzania na Afrika. Alikuwa mstahimilivu. Aliwatia watu moyo ili wakue kufikia mafanikio.

Mke wake, Lucy, amepoteza mume mpendwa sana. Harun Weggoro amempoteza baba anayejali. Mimi nimempoteza kaka mkubwa, rafiki na 'mentor'. Taifa letu limempoteza askari mpiganaji, mzalendo na kiongozi mashuhuri aliyeongoza akiwa nyuma ya pazia.

Nyota iliyong'aa sana imezima. Lakini aliyoyafanya ambayo yameiletea sifa nchi , Afrika Mashariki na Afrika yataendelea kuishi.

Wanafunzi wenzako uliokuwa nao Ujerumani, kama Prof. Paramagamba Kabudi na Dk. Harrison Mwakyembe watakulilia sana kaka.

Basi, nenda Kaka. Baba Mungu, mwingi wa rehema, akurehemu Dk. Namajeje Calleb Weggoro. Asante kwa kuwa baraka katika maisha yetu.

Sasa umetangulia. Nasi tutakufuata mmoja mmoja kadri alivyopangiwa na Mwenyezi Mungu. Tutaonana tena mahali ambapo hatutaagana tena.

Ulale kwa amani mzalendo. Ulitumia muda wako vizuri duniani. Pumzika Kaka. Pumzika kiongozi. Baba Mungu akuangazie nuru yake katika giza totoro. Lala kwa amani Kaka. **Tutaonana tena. Amina.**

MAKALA

## ILIVYOKUWA ZAMANI, LEO & YAJAYO...

# Mitindo ya nguo, nywele, viatu vya zamani inarejea?

**Na Adam Fungamwango**

KUMEKUWA na dalili zote kuwa baadhi ya mitindo mbalimbali ya zamani ya nguo, viatu, nywele inaanza kurejea taratibu, hata mitindo yao ikaendana.

Baadhi ya wataalamu wanasema hakuna mitindo yoyote ile mipya duniani. Ni kwamba inajirudia tu. Ni kama dunia inavyojizungusha kwenye mhimili wake.

Mfano mdogo tu kuna nguo za wanawake zamani zilikuwa zinaitwa 'max'. Ni nguo ndefu tu mithili ya shela iliyotamba kwenye miaka ya 1970, lakini ukiangalia leo hii ni kama mtindo huo wa nguo umerejea kwa sababu kinadada na kinamama wengi sasa wanapenda sana kuvaa nguo ndefu.

Tena zipo za aina mbalimbali, ikiwemo madera na vijora. Ni moja ya nguo ndefu ambazo zinapendwa sana na wanawake wengi kwa sasa. Ni ndefu kupita hata urefu wao, kiasi kwamba wakitaka kutembea ni lazima wayashikilie na mkono mmoja.

Mtindo mwingine ni huu wa vijana wa sasa wanaovaa mashati, fulana na suruali za kubana, wenyewe wanaziita 'modo'.

Wala si mavazi mapya. Miaka ya 1970, wakati vijana wanavaa suruali chini pana aina ya 'pekosi', ilikuwa ni lazima juu avae shati ya kubana ambalo huko nyuma wao waliyaita 'slim fiti'.

Hata hivyo, pekosi ilikuwa na ndugu yake 'bugaluu', ambayo upana wake ulianzia mapajani, huku pekosi upana unaanzia kwenye magoti. Ili 'kumechisha; ni lazima kuvaa viatu vilivyonyayuka juu aina ya 'raizoni', ambazo kulikuwa na mitindo yake; ngazi mbili, tatu hadi nne.

Halafu mwanzoni mwa miaka ya 1980, wakati enzi wa 'pekosi' inaisha, uliibuka mtindo wa suruali za kubana, zinaitwa 'don'touch', waswahili wenyewe wakaita 'dontachi'.

Jina hilo linaanzia mbali sana, kwani inadaiwa suruali ya mtindo huo, haikutakiwa kugusa kiasi chini, kwa hiyo kirefu ikajulikana kama 'don't touch my shoes', kwa hiyo ikaenda hadi ikafupishwa tu 'dontachi', aina ya mtindo unahusudiwa sana na msanii Diamond Platnumz, ukiwamo umma wa wafuasi inaomuiga kimavazi, wakiwamo wanafunzi.

Mtindo kama huo wa suruali za kubana hata kutamba zama hizo za miaka 1970 ukaitwa 'tinabul', lakini hii iliweza hata kugusa kiatu chini, lakini muundo wake inabana mwili.

Mtindo ambayo inaonekana kugoma kurudi ni mavazi ya khaki na kaniki. Mavazi haya tutazunguzia kwenye mada nyingine baadaye.



Ndivyo walivyovaa watanashati 'mabitoz' wa zama hizo, wa kulia amevaa pekosi na kushoto ana 'bugaluu'chini wote wamekamilisha kwa viatu raizoni. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

Hata uaazi wa nguo fupi wa kinadada haukuanza leo. Zamani kulikuwa na 'mini skirt', lakini kwa sasa wanaita 'kimini'. Serikali ya Awamu wa Kwanza chini ya Rais Julius Kambarage Nyerere, alianzisha kampeni ya kupiga vita uvaaji wa nguo hizo na ikawepo operesheni ya kuzuia nguo hizo wakati huo, mwanzoni mwa miaka ya 1970.

Kuanzia hapo miaka ya 1970, kulikuwapo nguo za aina 'crimplin' na walivaa watu wenye pesa tu. Kumbuka wakati huo haya 'majinsi' hayakuwapo na ukimuona mtu amevaa nguo inayofanana na hiyo ambazo ziliitwa 'Lee', basi atakuwa ametoka Ulaya.

Baadaye ndio zikamiminika za mtindo huo, lakini aina za kama vile, 'jeans' na 'dengriz'. Nguo hizo zilipendwa zaidi na 'masela' wa wakati huo, walioitwa 'magangwe'.

Baadaye 'pekosi' kushika hatamu kwenye miaka ya 1970, hadi mwanzoni mwa miaka ya 1980, mitindo ya nguo na nywele ilibadilika, kutoka kuachia nywele nyingi, maarufu kama 'afro'.

Na mara zote ililetwa na wanamuziki mbalimbali duniani. Mfano kundi la muziki la 'The Beatles' lililoanzishwa huko Liverpool Uingereza, walichangia sana mtindo wa uvaaji 'pekosi' kiasi cha vijana wakati huo akivaa hivyo anaitwa 'Bitozi'.

Jina hilo limeendelea kutumiwa hadi leo, kijana wa sasa akiwa mtanashati atajiita au kuitwa 'tozi'.



Viatu virefu maarufu raizoni vilivyotikisa sana uvaaji wa zama miaka ya 1970.

Wakaja wanamuziki kima Pat Shange, Chicco Twala wa Afrika Kusini, Tchico Chicaya wa Congo Brazaville walisababisha uvaaji kubalilika.

Kwanza, vijana wakaanza kunyoa 'panki', kuchoma nywele, lakini pia kuleta mtindo wa suruali aina ya 'bagi', mchelemchele na mashati ya ujiuji, kabla ya kuingia aina ya bahama. Wakati huo mwanzoni mwa miaka ya 1980, kulikuja mashati ya juliana, ambayo yalijulikana zaidi kwa jina la mashati ya ndege.

Hapo unajipaka mafuta ya mgando Yolanda, Ashes, na Ashanti, ambayo yalikuwa yanawekwa kwenye mkebe na ukipaka unanukia wiki nzima, hakuna pafyumu hapo wala nini.

Kwa mwanamama, kuna kinachodumu hadi sasa khanga, lakini wakati huo uvaaji khanga ulikuwa umefika katika hatua ya juu kabisa, kuiendana na 'binamu' yake kitenge.Hapo vazi hilo la kitaifa kwa kinamama nchini si haba, Khanga zilitoka kwa hatua, kila kinachozalishwa kinatikisa umma. Hapo kuna fasheni maarufu kama Khanga za Mpunga Kisele; Khanga za Mombasa; na Kitenge cha Zaire.'

Wazalishaji wake nchini wakati huo kukiwapo utitiri wa viwanda vya nguo, vinakumbukwa maarufu kama Sunguratex na Kiltex, ambavyo vilikuwa Gongolamboto Mwisho wa Lami, Dar es Salaam, sasa vimeshatoweka.

Hiyo ikaendana na aina hata ya mitindo ya nywele maarufu na mkongwe, unaodumu hadi sasa 'twende kilioni'ukiwa ngazi ya juu katika miaka ya 1970, huku kinachotamba leo 'raf dredi'kinamama zetu ndio ilifika mahali pake.

Upande wa viatu kulikuwa na 'skuna', 'raba mtoni', ndula kwa upande wa magangwe. Hii ni aina ya viatu vya ngozi, vikubwa na vigumu mithili ya viatu vya jeshi. Vote sasa vimerudi sokoni hasa katika upatikanaji viatu mtumba.

Kulikuwa na viatu vya pastiki, maarufu kama chachacha na vingine vya kutumbukiza, lakini ikifika saa sita vinaunguza mno, vijana wakaviita 'saa sita utanikoma'. Haijaeleweka kwanini, kwa sasa vinapedwa zaidi na makondakta wa daladala na jamii ya Wamasai.

Viatu vingi vilikuwa vinatengenezwa na kampuni ya Bora, pia Moro Shoes, huku vingine vikitengenezwa kienyeji tu, watoto wa mjini wakavibatiza jina la 'asante mchaga' na makala hii haitaisha bila kuzitaja aina fulani ya sendo zinazofanana na kandambili, lakini hizi zikichongwa kwa kutumia matairi ya gari. Ama kweli tumetoka mbali! Ahsanteni.

**Mawasiliano kwa sms: (+255) 716 350534).**

## Jeshi la Marekani laonya uasi Ethiopia

**Djibouti City,** DJIBOUTI

MWANAJESHI wa ngazi ya juu katika jeshi la Marekani barani Afrika, ameonya kuwa matukio ya uasi yanayotokea nchini Ethiopia, yanaweza kuathiri usalama wa maeneo mengine.

Katika mahojiano na BBC, Jenerali William Zana, alieleza kwamba Ethiopia ina wanajeshi katika nchi jirani ya Somalia wanaounga mkono serikali ya huko, hivyo wanaweza kuathirika.

"Ethiopia inapokuwa na mzozo wa ndani ambao unaweza kuifanya iamue kuondoa majeshi kutoka Somalia, sasa una nchi tano za Umoja wa Afrika ambazo pia zimeathirika na hali inayoendelea nchini humo kama Somalia kuna uwezekano wa mashirika yenye itikadi kali kuwa na shughuli kubwa zaidi huko," alisema.

Akizungumzia uwezekano kwamba mji mkuu wa Ethiopia, Addis Ababa, unaweza kulengwa na waasi wa Tigray, Jenerali Zana alisema kuwa jeshi la Marekani ambalo liko Djibouti liko tayari kuwahamisha raia wa Marekani.

Pia alielezea wasiwasi wake kuhusu uwezekano wa kuchukuliwa hatua za kijeshi na Misri dhidi ya bwawa kuu la Renaissance la Ethiopia, huku ukosefu wa utulivu Ethiopia unavyozidi kuongezeka.

**BBC**

## Uingereza yasitisha mpango kuwaajiri wauguzi kutoka Kenya

**LONDON,** UINGEREZA

SERIKALI ya Uingereza imesitisha mpango wa kuwasajili na kuwaajiri wauguzi kutoka Kenya.

Uingereza kupitia idara yake ya Afya, ilisema kwamba hakuna haja ya kuwaajiri wauguzi zaidi kutoka Kenya, wakati nchi hiyo ina uhaba wa wafanyakazi hao.

Hatahivyo, wauguzi ambao walikubaliwa katika maombi yao ya kazi kwenda nchini humo kufanya kazi hawataathiriwa na agizo hilo jipya.

Hata hivyo, Uingereza imesisitiza kutafanya uchunguzi zaidi ili kubaini ni nafasi ngapi za kazi zitahusishwa katika mpango wa ushirikiano wa mataifa hayo mawili kwa kuzinufaidisha nchi zote mbili.

Hatua hiyo inaonekana kama pigo kwa maelfu ya wauguzi nchini Kenya ambao walitarajiwa kuhamia Uingereza kufanya kazi.

Kenya na Uingereza zilifikia makubaliano kuhusu uhamiaji kwa lengo la kufanya kazi miongoni mwa wauguzi wakati Rais Uhuru Kenyatta alipozuru nchini Uingereza mwezi Julai 2021.

Makubaliano hayo yalitiwa saini na waziri wa Afya wa Uingereza Sajid Javid na mwenzake wa kazi wa Kenya Simo Chelugui.

Chini ya makubaliano hayo , wauguzi wasio na ajira nchini Kenya walihitajika kufanya kazi katika sekta ya huduma ya afya nchini Uingereza ya NHS kabla ya kurrejea nchini mwao. **BBC**

# Rais Nyusi amteua waziri mwanamke kuongoza Wizara ya Mambo ya Ndani

**MAPUTO,** MSUMBIJI

RAIS wa Msumbiji, Filipe Nyusi, amefanya uteuzi wa mwanamke wa kwanza kushika nafasi ya waziara ya mambo ya ndani.

Waziri huyo mpya ametajwa kuwa ni Felicidade Felix Massinge, ambaye ana uzoefu wa siku nyingi katika jeshi la polisi nchini humo.

Uteuzi huo umekuja siku chache baada ya kuwatimua kazi Waziri wa mambo ya ndani na waziri wa ulinzi.

Rais Nyusi, pia amemteua Cristóvão Artur Chume kwa Waziri wa Ulinzi.

Chume ni Meja Jenerali anayejulikana kwa kuongoza vikosi vilivyokomboa miji mingi, ikiwa ni pamoja na Mocimboa da Praia katika jimbo la Cabo Delgado lililoathiriwa na wanajihadi.

Massinge kabla ya kuteuliwa kwake alikuwa Kamishna Mkuu wa Uhamiaji.

Huko nyuma alikuwa Kamanda wa Polisi katika mikoa ya Inhambane, Manica na Nampula.

Rais Nyusi anatarajia kutumia uzoefu wake serikalini kukabiliana na changamoto zilizomuondoa madarakani mtangulizi wake, ikiwamo vitendo vya ugaidi, ufisadi na utekaji nyara.

**BBC**



Wafanyakazi wa shamba la ufugaji wa kamba katika kijiji cha Lambung nchini Indonesia wakiandaa samaki hao kwa ajili ya kwenda kuwauzia wateja. **PICHA: EPA-EFE**

# Al-Buruan ajitangaza kuongoza Sudan

**KHARTOOM,** SUDAN

KIONGOZI wa mapinduzi ya Sudan, Abdel Fattah al-Burhan, amelitaja baraza jipya la mawaziri na kujitangaza kuwa kiongozi wa muda.

Katika baraza hilo jipya, viongozi wa kiraia waliokuwa kwenye baraza lililopita wameondolewa.

Jenerali Burhan alibaki na makamu wake Mohamed Hamdan Dagalo, maarufu kama Hemeti, pamoja na viongozi wengine wakuu wa kijeshi ndio wamebaki na nyazifa zao walizoshikilia kabla ya mapinduzi ya Oktoba 25, mwaka huu.

Baraza hilo la mpito lenye wanachama 14, pia linajumuisha raia lakini hakuna hata mmoja kutoka muungano wa kisiasa uliokuwa madarakani kabla ya mapinduzi.

Waziri wa Habari wa Sudan, aliyeondolewa madarakani Hamza Balloul, aliitaja hatua hiyo mpya kuwa ni kurefusha muda wa mapinduzi.

"Watu wanaweza kuyashinda na kuendeleza kipindi cha mpito" alisema waziri huyo..

Baraza hilo jipya linakuja wakati kuna ongezeko la shinikizo la ndani na nje kutaka kugeuza mapinduzi hayo.

Mjumbe wa Umoja wa Mataifa nchini Sudan, Volker Perthes, alisema uteuzi wa mkuu wa jeshi wa upande mmoja wa baraza hilo unazidisha ugumu kwa nchi hiyo kurejea kwa utaratibu wa kikatiba.

Mjumbe huyo wa Umoja wa Mataifa alitoa wito wa kupatikana kwa suluhisho la dharura la mazungumzo ili kurejesha maisha ya kisiasa na kiuchumi katika hali ya kawaida.

Pia aliwataka wanajeshi kuchukua hatua nyingine za kujenga imani, ikiwa ni pamoja na kurejeshwa kwa uhuru kamili wa Waziri Mkuu Abdalla Hamdok.

**BBC.**

## Ethiopia itaendelea kuwakamata wafanyakazi Umoja wa Mataifa

**ADDIS ABABA,** ETHIOPIA

SERIKALI ya Ethiopia, imehidi kuendelea kuwakamata wafanyakazi wa Umoja wa Mataifa na Umoja wa Afrika ambao ni raia wa nchi hiyo iwapo watavunja sheria.

Tamko hili linakuja baada ya kukamatwa kwa wafanyakazi wa Umoja wa Mataifa kwa makosa ambayo hayajawekwa wazi. Watumishi saba kati ya waliokamatwa, waliachiwa huru na polisi, huku wakisisitiza kamata kamata hiyo haikuchochewa na ukabila.

Raia wa kigeni pia wamejikuta katika wimbi hilo la kamata kamata.

Serikali za Uingereza na Marekani zimesema raia wake kadhaa wamekamatwa na wako katika mazungumzo na serikali kuhusiana na suala hilo.

Ethiopia ilitangaza hali ya dharura mnamo Novemba 2, mwaka huu baada ya wapiganaji Tigray kuchukua udhibiti wa maeneo kadhaa na kutishia kuingia katika mji mkuu Addis Ababa.

**DW**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NYUMBA INAUZWA.

Ipo Pugu kajiungeni wilayani Ilala. Ina vyumba 3 vya kulala na sebule. Ujirani mzuri. Bei sh.15m tu.

**Simu 0782 574 669, 0621 879 477**

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.
MOB: +255 - 0782253676

## KUPOTEA KWA CHETI



**JACKLINE STEVEN THOMAS** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S2315-0053** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary **KANDOTO SAYANSI GIRLS mwaka 2016,** yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa **DAR/URA/RB/536889/2021**

## KUPOTEA KWA CHETI



**AGNES ROGASIAN ASSENGA**
Anatangaza kupotelewa na cheti chake cha under graduate certificate Kilichotolewa na chuo cha SUA kwa yeyote atakae ona au kuokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
**Rb Namba.MOR/MOR/RB/540098/2021**

**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA
AT DODOMA
(EXTENDED JURISDICITON)
SENIOR/PRINCIPAL PRM MISCELLAOUS
LAND APPEAL NO 8 OF 2021
HIGH COURT DC LAND APPEAL CASE NO.23 OF 2020
EDWARD NKANGA APPELLANT/APPL
VERSUS
MATHIAS SASII RESPONDENT
TO. MATHIAS SASII**

**NOTICE OF DATE OF HEAR/MENTION.**
**TAKE NOTICE** that the above case has been fixed for/hearing/mention on 08 day of DECEMBER 2021 at 9:00am.
**Before Hon. S.S LUSHASI, SRM**
**YOUR ARE** required to appear in his Court on the fixed date without fail. And you may bring with you all required document in support of your case.
Given under my hand and the seal of the Court this 10 day of 11 2021.

………………………………………………
**RESIDENT MAGISTRATE**

**IN THE COURT OF DISTRICT
DELEGATE OF MOROGORO
DISTRICT AT MOROGORO
PROBATE AND ADMINISTRATION
CAUSE NO 48 OF 2021**

**In the Matter of the Estate of the Late
ELIZABETH GORDEN
BY 1. GORDEN MPEMBWA
2. ……………………………….**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above – named petitioner.
Objection to the grant should be filed on or before the 18 day of 11….2021
Dated at Morogoro this 4 day of 11…..2021

RESIDENT MAGISTRATE

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

NOEL NDESARIO SWAI anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya GUTA yenye namba za usajili MC 796 DBA. Chassis No.1W8hd-nz41mw034845, Engine No. wh17mm-b210655427.Yeyote atakae iona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi DOD/-DOD/RB/538846/2021.

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA
AT DODOMA
PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.150. 2021
IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE AMOS LUGAKINGIRA
AND
IN THE MATTER OF AN APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY JOYCE EZEKIEL MUTOKA
GENERAL CITATION**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before 26 Day of 11,2021.
Dated at Dodoma this 18TH day of 11, 2020

………………………
**RESIDENT MAGISTRATE**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

DAUDI ABASS DAUDI anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya TOYOTA RAUM yenye namba za usajili T 805 CVG chasis namba NCZ200066196 engine namba 1NZB484128,yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa ARU/ARU /RB/539869/2021

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA
Katika mahakama ya mwanzo ya Wilaya ya ………..TANGA
Kituo cha….. MJINI TANGA…. Mkoa… TANGA
Usimamizi wa Mirathi…………198…………2021
KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA
MAREHEMU: HALIMA HUSSEIN OMARY
KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA
MSIMAMIZI YALIYOLETWA
NA: BAKARI ALLY SESE**

**TANGAZO**
***(Kanuni ya 5(2) ya kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)***
Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote/maslai yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 3/12/2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa.
Tarehe 12/11/2021

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA
Katika mahakama ya mwanzo ya
Wilaya ya Njombe
Kituo cha Njombe mjini
Mkoa njombe
Usimamizi wa mirathi na 48/2021
Emmanuel Andrew kachewa……marehemu
Nathalia Sabas Maqway………msimamizi**

**TAARIFA KWA UMMA**

**MAOMBI YA KUTANGAZA KUFUNGA MIRATHI**
Kwa wote wanaodai kuwa na haki na marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia orodha ya mali za marehemu na hesabu za mirathi katika jalada la mirathi
Mapingamizi yoyote kuhusu orodha ya mali na au hesabu za mirathi yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya siku ya tarehe 17th ya mwezi wa desemba mwaka 2021
Imetolewa na hakimu mkazi leo siku ya tarehe 12th novemba mwaka 2021

**Hakimu Mkazi**

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA
AT DODOMA
PROBATE AND ADMINISTRATION
CAUSE NO.157 OF 2021
In the matter of the Estate of the late
GODFREY ALINANINE SEME
Of Ndachi B within Dodoma City
And
In the matter of application for letters of Administration by LYDIA GODFREY SEME**

**GENERAL CITATION
(Rule 75 of Probate Rules Gn.369 of 1963)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 15/11/2021.
**Dated at Dodoma this 09/11/2021.**

RESIDENT MAGISTRATE

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe
MWANGA WA JAMII

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

## Namsaka mke wangu-19

**Mtunzi anapatikana (0716 350534)**

**Na Adam Fungamwango**

***TOM alipooa alidhani kuwa ataishi kwa amani, furaha na kupata utulivu kama inavyokuwa kwa rafiki na wenzake wote waliofanya hivyo.***

***Siku zote ndoa ni masikilizano, maelewano, na anayeoa hupata furaha na heshima. Kinyume chake, kwake amekuwa ni misukosuko, mikosi na balaa. Badala ya kuwa na ndoa yenye furaha, akajiingiza kwenye mtego hatari ambao hata baada ya kuufahamu, hakuweza kuutegua tena. Alichelewa. Ukawa ni mwanzo wa vilio, maafa na mtiririko wa mambo ya kushangaza.***

***Hebu pata kila nakala ya gazeti hili kufuatilia kisa hiki cha kushangaza na kusikitisha.***




WAKATI huo basi ilikuwa limeshafika Kibamba na wapenzi wao wawili waliteremka.

Wakakodisha taxi ya kuwapeleka nyumbani kwa Tom. Ni wakati ambao meseji nyingine ndefu iliingia.

Ilitoka kwa yule yule. "Mimi ni mtu mzima sasa. Nilivyoangalia niliona kabisa wewe na huyo dada aliyekuja hapa mna mahusiano. Sijui kama ni askari kweli au la. Nilivyomuona na yale maswali yake kama ni afande. Lakini kuna vitu nimeviona vinaniashiria kuwa ni wapenzi. Na mnapendana. Ni mwanamke mzuri, mrembo unaweza kumuoa. Mimi nimekwama. Haiwezekani tena. Dunia haitonielewa. Na wala wewe hutoeleweka. Ila tu naomba kama itawezekana muoe huyo dada." Ilimaliza meseji ya pili ambayo iliwashangaza kuliko ile ya kwanza.

Ni meseji ambayo ilimliza Tedi. Hata mwenyewe hakujua analia nini. meseji ya Farida imemliza, au ni machozi ya furaha baada ya kuonyeshewa taa ya kijani.

Ilibidi sasa Tom apate kibarua cha kumbembeleza. Wala hakutaka kumuuliza kinachomliza.

Msichana kutoka Singida, aliyepitia misukosuko kwenye maisha yake, akaenda Morogoro kusaka maisha. Akaangulia kuwa mhudumu wa baa akisumbuana na walevi wa kila aina na tabia za kila namna. Lengo ni kufanya kazi hiyo na kucheza upatu ili apate ada ya kujiunga na chuo cha urembo. Wakati anaanza kudunduliza anaangulia kwa mwanaume mmoja aliyetaka kupitisha naye usiku mmoja, lakini usiku unazaa siku na wiki kadhaa. Mbali na kazi aliyochukuliwa, anatumwa kazi moja ya hatari ya kumfuatilia mtu, kumelewesha na kumchukulia simu na nyaraka kadhaa. Anaifanikisha, akiwa anaifanya kwa ujira ya kulipiwa ada ya chuo cha urembo.

Hayo yote yamepita, lakini ghafla anaambiwa asirudi tena Singida, badala yake waongozane kwenda Dar es Salaam. Jiji ambalo hakuwahi kuliona, badala yake alikuwa anasimuliwa na baadhi ya wenzake aliokuwa akisoma nao wakienda kwa ndugu zao likizo.

Leo yupo Dar. Ni kama ndoto. Wakati akishangaa, inaonekana kabisa anaweza kuolewa na kuwa mama mwenye nyumba.

Tena na mwanaume ambaye ametokea kumpenda. Mwanaume ambaye tangu awe naye alijitofautisha na wengine ambao kazi yao, ilikuwa ni kumtumia tu kama ganda la mua na kumuacha akiteseka na ndoto zake za maisha ya baadaye, akiwa hajui maisha yake ya baadaye yatakuwaje.

Alichobakisha hapo Tedi ni kusikia kauli ya Tom tu. Ingawa alimwambia anataka awe mke wa pili, lakini aliona huo ulikuwa ni utani wa siku zote, kwani tangu akutane naye aligundua kuwa pamoja na ucheshi, alikuwa na utani.

"Sijamfanya chochote kibaya. Sijafanya dhambi kubwa kwa mwenyezi Mungu ambayo haisameheki. Mungu nisaidie kama ni kweli hili linataka kutokea iwe kweli." Aliomba kimoyomoyo Tedi.

"Mimi ni mtu mzima sasa. Nilivyoangalia niliona kabisa wewe na huyo dada aliyekuja hapa mna mahusiano. Sijui kama ni askari kweli au la. Nilivyomuona na yale maswali yake kama ni afande. Lakini kuna vitu nimeviona vinaniashiria kuwa ni wapenzi. Na mnapendana. Ni mwanamke mzuri, mrembo unaweza kumuoa. Mimi nimekwama. Haiwezekani tena. Dunia haitonieleiwa. Na wala wewe hutoeleweka. Ila tu naomba kama itawezekana muoe huyo dada."

Meseji hiyo ilikuwa ikirudia kichwani kwake. Ni meseji iliyoandikwa na Farida, mke wa Tom.

Na si Tedi tu. Hata Tom alikuwa mara kwa mara akiirudia kuisoma.

Alimsifu mkewe Farida kimoyomoyo kuwa ni mtu mwenye uwezo mkubwa wa kuhisi jambo.

**Sijamfanya chochote kibaya. Sijafanya dhambi kubwa kwa mwenyezi Mungu ambayo haisameheki. Mungu nisaidie kama ni kweli hili linataka kutokea iwe kweli.**

"Kwa kuhisi kuwa mimi na Tedi ni wapenzi, namsifu kwa hilo." Alijiambia.

Tayari walikuwa wameshafika nyumbani kwa Tom. "Karibu nyumbani." Tom alimkaribisha Tedi.

"Nashukuru." Alijibu kwa utulivu.

Ni nyumba iliyoonekana kabisa kuwa wenyewe waliondoka kwa muda kidogo, kwa sababu ilikuwa haina usafi.

Tom alitumia kama dakika 10 hivi kumzungusha kwenye nyumba na kumuonyesha mazingira yote ya ndani, pamoja na jiko.

"Natumai leo mchana nitaanza kula mapishi yako." Tom alitania, lakini na ukweli ndani yake.

"Akaa, sipiki. Umenishtukiza. Naweza kupika ugali haujaiva ikawa ndiyo tiketi yangu ya kurudi Singida." Naye alirudisha utani, ulimalizika kwa vicheko.

"Tena umenikumbusha, muda sasa sijala ugali, leo nataka ugali na dagaa."

"Umechoka na zile supu na chapati ya kule Morogoro ee." Tedi alizidi kutania.

"Tedi?" Aliita Tom.

"Abee." Alitikia kwa utulivu.

"Naweza kusema, wewe ndiye mke ambaye nimepewa na Mungu na si Farida."

Ni maneno yaliyomshtua Tedi na kumfariji kwa upande mmoja.

"Kwa nini unasema hivyo?"

"Kwanza umenisaidia sana kule Morogoro. Umekuwa mwenyeji wangu. Nilitoka Dar nina mawazo sana, lakini wewe ukayafuta mawazo yote. Wala sipati picha kama nisingekutana na wewe. Naona mwenyewe Farida ameamua kusalimu amri. Kwa yote yaliyotokea, nadhani haikuwa riziki yake. Ilikuwa ya kwako. Ndiyo maana unaona nimetoka Dar peke yangu kwenda kutafuta Farida. Lakini nimerudi na wewe. Na yote yaliyotokea kule, inaonyesha kabisa kuwa mke wangu halisi si Farida. Ni wewe."

"Nakubali, lakini kumbuka mpaka sasa hujamuacha Farida."

"Hilo niachie mimi. Yeye mwenyewe ameshaandika kuwa nikuoe wewe, nitamalizana naye, baada ya hapo nitaanza kufuata taratibu zingine za kukufanya mke."

Furaha aliyokuwa nayo Tedi ilimfanya ashinde kuzungumza.

Tom alimtazama Tedi. Aliona kabisa kuwa ndiye mke wa maisha yake. Akamkumbatia na kumbusu.

"Nakupenda sana Tedi."

"Nakupenda pia Tom wangu."

**MWISHO**

# KMC YAJIPANGA KUANZA LIGI IKIWAALIKA AZAM FC

**Na Saada Akida**

KATIKA kuhakikisha timu yake inajiweka katika nafasi nzuri kwenye msimamo wa Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara, Kocha Mkuu wa KMC FC, Habib Kondo, amesema anatarajia kupata matokeo mazuri kwenye mechi yao dhidi ya Azam FC itakayochezwa Novemba 21, mwaka huu kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.

**Akizungumza na gazeti hili jana, Kondo alisema wamejipanga kuendeleza ushindi dhidi ya Azam na anaamini wachezaji wake watacheza kwa umakini kwa ajili ya kutimiza malengo yao.**

Kondo alisema wanawafahamu vyema wapinzani wao na wataingia uwanjani katika mechi hiyo wakiwa hawana wasiwasi wowote.

"Tumejipanga kuifungia kazi Azam FC, kwa kifupi tunataka kuendeleza ubabe dhidi ya Wana-lambalamba hao katika mchezo huu wa kwanza msimu huu," alisema Kondo.

Kocha huyo alisema anatambua ligi ya msimu huu ina ushunda mkubwa na hivyo wanatakiwa kujiandaa vyema na hatimaye kuendeleza rekodi safi ya kuondoka na pointi tatu wakiwa nyumbani.

"Hakuna mechi rahisi msimu huu, tunajua kila timu imejipanga, kikubwa ni wachezaji kutulia na kutekeleza yale tunayowapa mazoezini," Kondo alisema.

Aliongeza wakati ligi ikiwa imesimama kupisha kalenda ya kimataifa, wachezaji wake waliendelea na mazoezi na alitumia muda huo kufanyia kazi upungufu na pia kujiimarisha zaidi kwenye maeneo.

"Hatukuwa na mapumziko kwa sababu hatukuanza na mwenendo mzuri msimu huu, upungufu mwingi umejitokeza lakini pia kuna mechi ngumu mbele yetu dhidi ya Azam, tunahitaji kuendeleza rekodi yetu nzuri ya kuvuna pointi tatu mbele yao," alisema Kondo.

Alisema msimu huu ni mgumu kuanzia mechi za awali na wanatakiwa kujiimarisha zaidi kwa sababu timu zote zimetumia vyema mapumziko kujenga vikosi vyao.

Katika msimamo wa Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara ambayo itaendelea tena kuanzia Novemba 19, mwaka huu, KMC FC yenye pointi mbili inashika nafasi ya pili kutoka mkiani.

Yanga yenye pointi 15 ndio vinara wa ligi hiyo wakati wanafuatiwa na mabingwa watetezi ni Simba, wenye pointi 10 kibindoni.




Wanamuziki wa bendi ya Moro Jazz, Papaa Fani (kushoto) na Ally Yahaya wakitoa burudani katika maadhimisho ya Kutambua Watoto Mapacha yaliyoandaliwa na Shirika lisilo la kiserikali la Eden Twins Foundation jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA : SABATO KASIKA**

# *Da Cruz awafunda wasanii nchini*

**Na Faustine Feliciane**

WASANII wa sanaa ya uchoraji nchini wametakiwa kubuni na kufanya kazi kwa kujituma ili kujitangaza na hatimaye kupata masoko ya kimataifa ya kazi zao badala ya kukaa na kusubiri 'michongo', imeelezwa.

Kauli hiyo ilitolewa jijini Dar es Salaam jana na msanii wa kimataifa wa uchoraji wa mtindo, Graffiti Da Cruz kutoka nchini Ufaransa.

Da Cruz ambaye ameungana na Kundi la 'Wachapa' la hapa nchini kwa ajili ya kufanya kazi mbalimbali, alisema endapo sanaa itatumika vizuri, basi ni fursa kwa vijana lakini inahitajika kujituma na kuongeza ubunifu.

Aliongeza tangu amefika Tanzania amejifunza sanaa mbalimbali ambazo hakuzifahamu kabla ya kuja nchini.

Naye mmoja wa wasanii wa Kundi la Wachapa, Mawila Khamais 'Localfanatics', alisema wanajifunza mengi kupitia msanii huyo na ujio wake utakuwa na faida zaidi kwao.

Mkurugenzi wa Kituo cha Utamaduni cha Ufaransa, ambao ndio wamemleta nchini msanii huyo, Flora Valleur, alisema ili kukuza utamaduni na kujenga daraja kati ya sanaa za mitaani hapa jijini na Ufaransa, Alliance France imezindua mradi wa D'Art ambao utawawezesha wasanii wa sanaa ya uchoraji kujenga mazoea ya sanaa hiyo.

"Mradi huu ulikuwa na awamu tatu na ulianza tangu Oktoba 30, mwaka huu, na hii ni awamu ya mwisho ambayo tumeshuhudia ujio wa Da Cruz, tunaamini kwa kushirikiana na wasanii wa hapa nchini watabadilishana maarifa na kuendeleza sanaa hii," alisema Flora.

# Mashujaa, Kitayosce mchuano wa majirani

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Kitayosce, Fulgence Novatus amesema kikosi chake kiko kamili na imara kuwakabili wenyeji wao, Mashujaa FC katika mechi ya Ligi ya Championship itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika mkoani Kigoma.

Fulgence aliliambia gazeti hili jana kikosi chake kimejiandaa vizuri na kila mchezaji yuko tayari kupambana ili kuondoka na ushindi wa ugenini.

Kocha huyo alisema kila mechi wake ni sawa na fainali na wamejiandaa kuhakikisha wanapata pointi tatu muhimu na hatimaye kuendelea kujiimarisha katika msimamo wa ligi hiyo inayochezwa kwa mfumo wa nyumbani na ugenini.

"Tumefika Kigoma leo (jana) mchana, na wachezaji wote tuliokuja nao wako fiti, malengo yetu makubwa ni kuhakikisha tunapanda daraja, ingawa tunatakuwa wapinzani wetu nao wanahitaji matokeo mazuri, tunatambua mechi itakuwa ngumu na yenye ushindani mkubwa," alisema Fulgence.

Aliongeza wanatambua wenyeji wao watahitaji kutumia vyema uwanja wa nyumbani hivyo wataongeza umakini kuhakikisha wanaondoka Kigoma na furaha ya ushindi.

" Ni wazi kila upande umejipanga vizuri kutafuta matokeo chanya na kujiweka katika nafasi nzuri kwenye msimamo wa ligi hiyo. Naamini vijana wangu wakitulia, tutapata kile tulichokifuata katika mechi hii, ligi ni ngumu na kila timu inahitaji kupata ushindi mapema," aliongeza kocha huyo.

Katika msimamo wa ligi hiyo, Kitayosce yenye pointi 10 sawa na Mashujaa iko katika nafasi ya sita na inafuatiwa na wapinzani hao ambao ni 'Maafande' wa Kigoma.

Mechi nyingine za ligi hiyo itakazochezwa leo itakuwa ni kati ya Fountain Gate dhidi ya Mwadui FC wakati kesho Alliance FC watawakaribisha Mbao kwenye Uwanja wa Nyamagana.

DTB FC ya jijini Dar es Salaam ambayo ina pointi 14 ndio vinara wa ligi hiyo inayoshirikisha timu 16 huku African Lyon iliyopoteza mechi zote sita ikiburuza mkia.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### STERLING RASMI SOKONI

MANCHESTER City ipo tayari kumuuza mshambuliaji wake, Raheem Sterling na thamani ya mchezaji huyo wa kimataifa wa England imetajwa kuwa ni karibia pauni milioni 45. ***(Metro)***

### OLMO ANUKIA BARCELONA

BARCELONA inafakiria kumnunua, Raheem Sterling kwa mkopo ifikapo Januari, lakini pia ina hamu ya kumsajili kiungo wa kati wa RB Leipzig ambaye ni raia wa Hispania, Dani Olmo, 23. ***(Marca)***

### XAVI APEWA FUNGU

KOCHA mpya wa Barcelona, Xavi atakuwa na kitita cha fedha ili kuimarisha kikosi chake katika dirisha la uhamisho la Januari. ***(ESPN)***

### UNITED KUTIKISIKA

NEWCASTLE inawalenga wachezaji watatu wa Manchester United katika dirisha la Januari akiwamo, kiungo wa kati wa Uholanzi, Donny van de Beek mwenye miaka 24, kiungo wa kati wa England, Jesse Lingard (28), na kipa, Dean Henderson (24). ***(Mirror)***

### MADRID YAMTAKA NDIDI

REAL Madrid inamnyatia kiungo wa Leicester na Timu ya Taifa ya Nigeria, Wilfred Ndidi, 24, katika dirisha la uhamisho la Januari. ***(Leicestershire Live, via Fichajes)***

### BALE MAMBO MAGUMU

TOTTENHAM Hotspur haina mpango wa kumsajili winga wa Wales na Real Madrid, Gareth Bale, 32, licha ya kuhusishwa kwa mchezaji huyo. ***(Football London)***

### KULUSEVSKI ANUKIA SPURS

TOTTENHAM Hotspur ina hamu ya kumsajili winga wa Juventus, Dejan Kulusevski, 21. ***(Calciomercato)***

### ARSENAL YAINGIA SOKONI

ARSENAL inatajwa inamtazama, Dejan Kulusevski, ambaye amekuwa hachezeshwi mara kwa mara katika kikosi cha Juventus tangu kuanza kwa msimu huu. ***(Sky Italy)***

### GUENDOUZI AAMUA KUFUNGUKA

KIUNGO wa kati wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, Matteo Guendouzi, 22, anataka kusalia katika klabu ya Marseille wakati mkopo wake kutoka Arsenal utakapoisha. ***(RMC, via Mirror)***

### BARCA YAMTAKAA ALVES

BARCELONA haitamsajili upya beki wa kulia wa Timu ya Taifa ya Brazil, Dani Alves, ambaye ni mchezaji huru na amehusishwa na klabu hiyo. ***(Goal)***

### ADAMS AKARIBIA ARSENAL

ARSENAL ina nia ya kumsajili kiungo wa kati wa RB Leipzig na Timu ya Taifa ya Marekani, Tyler Adams, 22. ***(Mirror, via Sport Bild)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# JORGINHO AJIPANGA KULETA MAPINDUZI

**●●● Ni kuhusu mchezaji mwenye sifa ya kushinda tuzo ya Ballon d'Or...**

**LONDON,** England

KIUNGO wa Chelsea, Jorginho, anaamini kama akifanikiwa kushinda tuzo ya Ballon d'Or 2021, ataleta motisha kwa wachezaji wengine ambao si wafungaji.

**Na kwamba, itadhihirisha kigezo cha kutwaa tuzo hiyo sio uwezo wa kufunga mabao pekee.**

Jorginho ni mmoja wa wachezaji wanaowania Ballon d'Or ambapo anapewa nafasi kubwa ya kuibuka mshindi baada ya kuwa na msimu mzuri uliopita akifanikiwa kutwaa taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa na Chelsea na Kombe la Euro 2020 akiwa na Italia.

Nyota huyo mwenye asili ya Brazil aliibuka Mchezaji Bora wa Kiume wa mwaka wa Shirikiso la Soka Ulaya (UEFA), Agosti, mwaka huu baada ya kuisadia Chelsea kushinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya na Italia Euro 2020.

Jorginho ambaye amefunga mabao nane kwenye mashindano yote msimu huu anachuana na Robert Lewandowski na Lionel Messi ambao ndio wapinzani wakuu kwenye mbio za kuwania tuzo hiyo kubwa duniani.

"Sio suala langu kusema kama natakiwa kushinda Ballon d'Or, lakini italeta motisha kwa wachezaji wengine kuonyesha kwamba mabao sio kigezo pekee kinachozingatiwa," alisema Jorginho akinukuliwa na Sky Sport Italia.

"Ni wazi kwamba, tuzo hii imekuwa ikishindaniwa na wafungaji zaidi, lakini nafikiri ni wakati sasa wa kuangalia nafasi nyingine uwanjani."

MECHI KALI
HOME
AWAY
MONTENEGRO
10.97 | 5.78 | 1.26
NETHERLANDS

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#,
CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money ZANTEL EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

CHEZA USHINDE
JACKPOT TZS. 667



# LAMPARD, NORWICH RASMI KIMEELEWEKA

**LONDON,** England


FRANK Lampard yupo mbioni kutangazwa kama kocha mkuu wa timu ya Norwich City, muda wowote kuanzia sasa kutokana na uhitaji mkubwa wa klabu hiyo tangu kufuzwa kwa Daniel Farke.

Kocha wa zamani wa klabu za Derby na Chelsea anatarajia kubeba majukumu ya Farke, ambaye alifutwa kazi wiki iliyopita baada ya kupata ushindi wake wa kwanza dhidi ya Brentford.

Lampard amekuwa hana kazi tangu alipofungashiwa virago na Chelsea Januari, mwaka huu baada ya kuwa na matokeo mabovu na kutoka kwenye nafasi nne za juu hadi nafasi ya tisa.

Kwa sasa Lampard anajiandaa kubeba mzigo uliomshinda Farke wa kuitoa Norwich kutoka kwenye hatari ya kushuka daraja na kurudisha hamasa ya ushindi kwa wachezaji na klabu nzima kwa ujumla.

Kwa mujibu wa ripoti za nchini England, mabosi wa Norwich wanaona Lampard anaweza kuwanyanyua kutoka nafasi waliyopo hivi sasa.



# *Tite kicheko Brazil ikifuzu Qatar 2022*

**SAO PAULO,** Brazil

KOCHA Mkuu wa Timu ya Taifa ya Brazil, Tite, amesema Selecao hao wameonyesha kiwango cha kuvutia baada ya kukata tiketi ya kufuzu fainali za Kombe la Dunia zitakazofanyika mwakani nchini Qatar.

Bao la Lucas Paqueta la kipindi cha kwanza liliwawezesha kupata ushindi wa goli 1-0 dhidi ya Colombia hapo juzi na Brazil ikafuzu rasmi kwenda kwenye fainali hizo.

Ushindi huo umeifanya Brazil kushinda mechi 11 zilizopita za kufuzu na kuwa ushindi mrefu zaidi kuliko timu yoyote kutoka Mataifa ya Amerika Kusini.

Licha ya Brazil kupata tiketi hiyo, Tite amesema washindi hao mara tano wa Kombe la Dunia ha-

watapumzika k
mchezo wa Ju
dhidi ya wapinza
Argentina.

“Walicheza vi
bao la ushindi
zuri kabisa,” alise
akiwaambia wa
wa habari.

“Kwa uhakika
jambo zuri. U
ezaji wa bao na k
beki ilikuwa im
tumeshinda vizu
ndilo linalonifura

7,771,400

JACKPOT

MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 13/11/21 | 18:00 | Rochdale vs Leyton Orient | 2.27 | 3.28 | 2.99 |
| 02. 13/11/21 | 18:00 | Tranmere vs Sutton United | 2.32 | 3.23 | 2.94 |
| 03. 13/11/21 | 18:00 | Stevenage vs Mansfield | 2.46 | 3.20 | 2.76 |
| 04. 13/11/21 | 18:00 | Bristol Rovers vs Northampton | 2.41 | 3.19 | 2.85 |
| 05. 13/11/21 | 18:00 | Walsall vs Harrogate | 2.60 | 3.23 | 2.60 |
| 06. 13/11/21 | 18:00 | Altrincham vs Boreham Wood | 2.83 | 3.27 | 2.35 |
| 07. 13/11/21 | 18:00 | Yeovil vs Eastleigh | 2.38 | 3.22 | 2.83 |
| 08. 13/11/21 | 18:00 | Wealdstone vs Barnet | 2.43 | 3.41 | 2.63 |
| 09. 13/11/21 | 18:00 | Accrington vs Plymouth | 2.70 | 3.44 | 2.39 |
| 10. 13/11/21 | 20:15 | Mirandes vs Huesca | 2.34 | 3.14 | 2.99 |
| 11. 14/11/21 | 18:00 | UD Ibiza Eivissa vs Almeria | 3.13 | 3.18 | 2.24 |
| 12. 14/11/21 | 20:15 | Leganes vs Real Oviedo | 2.29 | 2.99 | 3.23 |
| 13. 14/11/21 | 20:15 | Burgos vs Ponferradina | 2.41 | 3.03 | 2.98 |


MECHI ZA USHINDI

“1” NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA “X” NI TIMU KUTOKA SARE
“2” NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAMOSI - 13 - NOVEMBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 15:00 | 2871 | Port Vale vs Bradford City | 2.18 | 3.29 | 3.15 |
| 15:40 | 4446 | AL Jazira AL Hamra vs Hatta Club | 3.85 | 4.05 | 1.69 |
| 15:40 | 4547 | Masafi vs AL-Rams | 1.11 | 8.09 | 13.49 |
| 15:45 | 5910 | Masfoot Sports Club vs AL Tawon SC | 2.01 | 3.72 | 3.00 |
| 16:00 | 3003 | Oriolik vs HNK Rijeka | 24.22 | 10.66 | 1.04 |
| 16:00 | 3341 | Zambia vs Mauritania | 1.59 | 3.48 | 5.41 |
| 16:00 | 4435 | Uhersky Brod vs FC Slovan Rosice | 2.51 | 3.71 | 2.31 |
| 16:00 | 4597 | Velke Mezirici vs Vratimov | 2.16 | 3.75 | 2.69 |
| 16:00 | 5316 | Malawi vs Cameroon | 11.64 | 4.66 | 1.25 |
| 16:00 | 5420 | Carlisle vs Barrow | 2.34 | 3.19 | 2.94 |
| 17:00 | 2332 | Bosnia and Herzegovina vs Finland | 2.05 | 3.29 | 3.74 |
| 18:00 | 1732 | Stevenage vs Mansfield | 2.46 | 3.20 | 2.76 |
| 18:00 | 1776 | Hamilton vs Raith Rovers | 2.93 | 3.22 | 2.31 |
| 18:00 | 1854 | Accrington vs Plymouth | 2.85 | 3.44 | 2.28 |
| 18:00 | 1964 | Tranmere vs Sutton United | 2.59 | 3.18 | 2.64 |
| 18:00 | 2659 | Wycombe vs Portsmouth | 2.06 | 3.34 | 3.39 |
| 18:00 | 2882 | Exeter vs Oldham | 1.72 | 3.67 | 4.40 |
| 18:00 | 3015 | Southend vs Woking | 2.27 | 3.37 | 2.88 |
| 18:00 | 3100 | Walsall vs Harrogate | 2.50 | 3.24 | 2.70 |
| 18:00 | 3113 | Rochdale vs Leyton Orient | 2.32 | 3.23 | 2.94 |
| 18:00 | 3380 | Kings Lynn vs Wrexham | 4.40 | 3.81 | 1.68 |
| 18:00 | 3408 | Wealdstone vs Barnet | 2.39 | 3.47 | 2.64 |
| 18:00 | 3847 | Arbroath vs Queen of South | 1.85 | 3.51 | 3.85 |
| 18:00 | 4323 | Valladolid vs Fuenlabrada | 1.51 | 3.94 | 6.11 |
| 18:00 | 4437 | Ayr United vs Partick Thisle | 2.88 | 3.17 | 2.36 |
| 18:00 | 4546 | Elgin City vs Cowdenbeath | 2.16 | 3.37 | 2.94 |
| 18:00 | 4640 | Burton vs Charlton | 2.55 | 3.29 | 2.60 |
| 18:00 | 4697 | Portadown FC vs Carrick Rangers | 2.83 | 3.55 | 2.15 |
| 18:00 | 4931 | Sheffield Wed vs Gillingham | 1.60 | 3.87 | 5.10 |
| 18:00 | 4992 | Aldershot vs Grimsby | 3.57 | 3.52 | 1.92 |
| 18:00 | 4999 | Ipswich vs Oxford Utd | 2.24 | 3.33 | 2.99 |
| 18:00 | 5012 | Inverness vs Dunfermline | 1.72 | 3.71 | 4.29 |
| 18:00 | 5025 | Chesterfield vs Weymouth | 1.37 | 4.60 | 7.24 |
| 18:00 | 5425 | Glentoran Belfast vs Ballymena Utd | 1.30 | 5.19 | 7.31 |
| 18:00 | 5787 | Morton vs Kilmarnock | 3.57 | 3.22 | 2.02 |
| 19:00 | 1718 | Equatorial Guinea vs Tunisia | 4.82 | 3.33 | 1.69 |
| 19:00 | 3825 | Liberia vs Nigeria | 14.44 | 5.01 | 1.20 |
| 19:00 | 4016 | Cape Verde vs Central African Republic | 1.54 | 3.53 | 6.00 |
| 20:00 | 4862 | Norway vs Latvia | 1.14 | 7.79 | 18.96 |
| 20:00 | 5556 | Turkey vs Gibraltar | 1.01 | 18.99 | 100.95 |
| 20:15 | 2543 | Eibar vs Alcorcon | 1.39 | 4.32 | 7.65 |
| 20:15 | 4678 | Mirandes vs Huesca | 3.05 | 3.10 | 2.32 |
| 20:20 | 1922 | Stockport vs Bromley | 1.89 | 3.57 | 3.62 |
| 22:00 | 4266 | Ivory Coast vs Mozambique | 1.18 | 5.40 | 15.43 |
| 22:30 | 2375 | Longford Town vs Waterford Utd | 5.20 | 3.86 | 1.54 |
| 22:30 | 3044 | Las Palmas UD vs Zaragoza | 2.02 | 3.05 | 3.88 |
| 22:45 | 1390 | Wales vs Belarus | 1.21 | 6.20 | 13.99 |
| 22:45 | 2503 | France vs Kazakhstan | 1.03 | 13.00 | 80.02 |
| 22:45 | 3027 | Belgium vs Estonia | 1.03 | 13.99 | 59.94 |
| 22:45 | 5552 | Montenegro vs Netherlands | 10.97 | 5.78 | 1.26 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# PJANIC AREJESHA MATUMAINI BARCELONA



**BARCELONA,** Hispania

NYOTA wa Barcelona, Miralem Pjanic, anaripotiwa kwa sasa ana matumaini ya mwanzo mpya baada ya kuwasili kwa Xavi kama kocha mpya wa timu hiyo.

Pjanic alijikuta analazimika kuondoka kwa mkopo kwenda Besiktas, ambako yupo sasa akianza msimu wake vyema baada ya changamoto za majeraha.

Nyota huyu mwenye miaka 31 aliwasili Barcelona mwaka 2020, ikiwa ni sehemu ya dili la kubadilishana wachezaji lililomhusisha, Arthur Melo. Kwa mujibu wa Mundo Deportivo, Pjanic sasa ana matumaini mapya juu ya hatima yake ndani ya klabu ya Barcelona.

Pjanic ni moja ya watu wanaomkubali zaidi Xavi, na anaamini atapata nafasi ya kumshawishi meneja huyu baada ya kumalizana na dili lake la mkopo huko Besiktas. Xavi kwa upande wake ameshawaahidi wachezaji kuwa yeye vigezo vyake vitakuwa ni ubora pekee, na hakuna jambo jingine.

Ikiwa nyota huyo atapata nafasi ya kumshawishi basi huenda akapewa nafasi ya kuthaminiwa zaidi hapo Barca.

...uelekea
...umanne
...ani wao

...zuri na
...lilikuwa
...ema Tite
...handishi

...lilikuwa
...Utengen-
...kufunga,
...nara na
...ri. Hilo
...ahisha.”



# Rodgers atajwa kumrithi Ole

**MANCHESTER,** England

HABARI za chini ya kapeti zinamtaja Brendan Rodgers kama kocha atakayepewa kibarua pale Old Trafford, kwa mujibu wa Daily Mail.

Rodgers aliwahi kufundisha Liverpool ambayo aliifikisha nafasi ya pili katika msimamo wa Ligi Kuu England msimu wa 2013/14.

Muda mfupi baadaye alijiunga na Celtic kabla ya mwaka 2019 kurejea kwenye Ligi Kuu England na kuichukua Leicester City ambayo bado yupo nayo.

Kinachoongeza matumaini kwa uwezekano wa kocha huyo kutua Old Trafford ni uwepo wa kipengele cha kimkataba ambacho, Brendan anaruhusiwa kujiunga na timu yeyote ambayo inacheza Ligi ya Mabingwa Ulaya (kama timu hiyo itamhitaji).

Bodi ya Wakurugenzi wa Manchester United bado haijatoa tamko rasmi kuhusu hatima ya Ole Gunnar Solskjaer, lakini kuna uwezekano kocha huyo akatimuliwa klabuni hapo muda wowote ndani ya msimu huu.

Michezo
Jumamosi Novemba 13, 2021
Nipashe



Jorginho ajipanga kuleta mapinduzi UKURASA 21

# Dakika 90 chungu zilizoimaliza Taifa Stars

## Sasa yajipanga kwenda kukamilisha ratiba kwa heshima dhidi...

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

MATUMAINI ya Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), kwenda kwa mara ya kwanza kushiriki fainali za Kombe la Dunia zitakazofanyika mwakani nchini Qatar zimefikia kikomo baada ya Benin kuichapa Madagascar mabao 2-0 katika mechi nyingine ya Kundi J iliyochezwa juzi usiku.

**Hata hivyo, Stars ilianza kupata 'uchungu' mapema kufuatia kichapo cha mabao 3-0 kutoka kwa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC), huku ikiwa nyumbani kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.**

Dakika hizo 90 za kwanza zilipoteza matumaini ya ndoto ya Stars kwenda katika fainali hizo, lakini baadaye ndoto hizo zikazimika kufuatia ushindi ambao Benin waliupata.

Kwa matokeo hayo, Stars sasa itawakabili Madagascar katika mchezo wake wa mwisho wa hatua ya makundi kwa kusaka heshima sawa na wenyeji wao ambao wanaburuza mkia kwenye kundi hilo.

Ikicheza nyumbani mjini Cotonou kwenye Uwanja wa L'amitie, Benin ilipa ushindi kupitia kwa wachezaji wake, Joden Dossou aliyefunga dakika ya 44 na muuaji wa Stars kwenye mechi iliyochezwa Oktoba 7 Uwanja wa Benjamin Mkapa, Steve Mounie alifunga goli la pili dakika ya 79.

Ni ushindi ambao umeondoa Tanzania yenye pointi saba hata kama itaifunga Madagascar itafikisha pointi 10 ambazo hazitasaidia kwa sababu zitapitwa kwa matokeo yoyote yale kati ya Benin dhidi ya DRC.

Kocha Mkuu wa Stars, Kim Poulsen, amesema licha ya kucheza na timu bora lakini kikosi chake hakikuonyesha kiwango kizuri kama ilivyofanya katika michezo miwili iliyopita ya mashindano hayo.

Poulsen alisema walikuwa na matumaini makubwa katika mchezo huo wa juzi, na kukiri walikutana na timu yenye nafasi nzuri katika ubora wa viwango ikiwa pia imejaa wachezaji wenye uzoefu.

Alisema timu yako inaweza kutengeneza nafasi nyingi lakini ikashindwa kuzitumia huku mpinzani wako akapata chache na akakuadhibu kwa makosa yao.

"Tulifanya makosa baada ya dakika sita na Congo wakatuadhibu kwa kuongoza bao 1-0, kwenye safu ya kiungo tulicheza vizuri, tulipoenda mapumziko tumechoka na kujipanga tena tumerejea tulifanya vizuri kisha dakika moja tunafanya kosa lingine na kuadhibiwa," alisema Poulsen.

Aliongeza timu yake ilitengeneza nafasi nyingi, ilipata kona na mipira ya adhabu ambayo walishindwa kuitumia jambo ambalo ni muhimu unapocheza katika mechi za kusaka tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Dunia dhidi ya timu iliyoko katika nafasi ya 67 kwenye viwango vya FIFA.

"Tujifunze kupitia upungufu na makosa yetu, kila mchezo tulionao tunachukuwa kama somo, nashukuru tulichojifunza kwenye mchezo wa leo (juzi), unapata majibu unapata maswali, tuko wapi kwenye safari yetu, tumejifunza ukitaka kushindana na timu ya kiwango cha juu huwezi kuruhusu nafasi yako kufanya makosa ya aina hii tuliyofanya leo," Poulsen aliongeza.

Alisema watafanyia kazi upungufu walioubaini ili kuhakikisha wanapata matokeo mazuri dhidi ya Madagascar licha ya tayari wameshatoka kwenye mbio za safari ya kuelekea Qatar.

"Tutaendelea kupambana katika mechi ya mwisho, tulikuwa tunaimani ya kupata matokeo mazuri na kufungua milango ya kwenda kucheza Kombe la Dunia lakini haikuwa bahati kwetu," alisema kocha huyo.

Mechi kati ya Stars na Madagascar itachezwa kesho wakati DRC itawakaribisha Benin jijini Kinshasa.



Kiungo wa kimataifa wa Yanga, Mukoko Tonombe, akijaribu kumiliki mpira katika mazoezi ya timu hiyo yanayoendelea kwenye Uwanja wa Amaan, Zanzibar kwa ajili ya kujiandaa na michezo ya Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara inayotarajiwa kuendelea kuanzia Novemba 19, mwaka huu. **PICHA: MTANDAO**

## Simba, Yanga kuinogesha Ilala

**Na Saada Akida**

MABINGWA watetezi wa Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara, Simba na Yanga zimethibitisha kushiriki katika Tamasha la Wiki ya Mkoa wa Ilala lililoandaliwa na Chama cha Soka Wilaya ya Ilala (IDFA), cha jijini Dar es Salaam, imefahamika.

Tamasha la Wiki ya Mkoa wa Ilala kwa upande wa mpira wa miguu limepangwa kufanyika kuanzia Novemba 15 hadi 21, mwaka huu.

Timu nyingine ya Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara iliyothibitisha kushiriki katika tamasha hilo la kwanza kufanyika nchini ni Azam FC.

Akizungumza na jijini jana, Mwenyekiti wa IDFA, Kondo Mussa, alisema katika tamasha hilo kutakuwa na matukio mawili yakiwamo kutoa msaada kwa wazee wasiojiweza, kutembelea watoto yatima walioko katika shule za msingi, waliolazwa hospitalini na kutoa misaada mbalimbali.

Kondo alisema katika kuadhimisha kilele cha wiki hiyo kutakuwa na burudani ya mechi ambayo itatoa mshindi.

Mwenyekiti huyo alisema katika tamasha hilo, Simba itacheza dhidi ya Boom FC wakati Yanga watakutana na Pan African huku Azam FC yenyewe itawakabili Ilala Kombaini.

"Kila mmoja atacheza siku yake, lakini pia kutakuwa na tuzo kwa klabu bora kwa timu hizo kongwe pamoja na mchezaji bora wa mashabiki," alisema kiongozi huyo.

Aliongeza Simba na Yanga watapewa tuzo kwa sababu ni timu zilizopo katika mkoa huo na wanaendelea kufanya vizuri katika mashindano mbalimbali ndani na nje ya Tanzania huku Azam FC ikipewa nafasi kwa sababu timu hiyo iliyoanzia mkoani humo kabla ya kuhamia Temeke.

"Malengo mengine ni kuwatambua wadau wa Ilala ambao wameufanya mkoa huu kufanya vizuri katika soka, walikuwa hawajakumbukwa kwa mchango wao, ila sasa tumewaandalia tuzo hizo," alisema Kondo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >